

**Unajua nini kuhusu changamoto maishani?**
Uk.8



**Limao ni dawa, kiungo na sharubati**
Uk.15



**Watu 11 wafariki dunia mgodini**
Uk.19

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo



Uk. 24

**Kumekucha Simba**

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00040 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Novemba 29 - Desemba 5, 2023 |

# Mashirika, taasisi 19 zakalia 'kuti kavu'


Uk.4

## Samia kuongoza vikao CC, NEC
Uk.4



## Tume ya Haki za Binadamu yatia mguu sakala la Pauline Gekul


Uk. 2

## Mtanzania aliyeuawa Israel kuzikwa leo Rombo
Uk. 5

## Wanaosubiri madawati, watasubiri wakiwa nje ya mfumo
Uk.3



## Katambi asisitiza uzalendo kwa vijana


Uk. 7



## Abiria kuchimba dawa sasa ni dakika 20

# Doto Biteko akutana na uongozi wa Chama cha Kikomunisti cha China



**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amekutana na kufanya mazungumzo na Uongozi wa juu wa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) ukiongozwa na Mjumbe wa Kamati na Mkurugenzi Mkuu wa Bureau I, Idara ya Oganaizesheni ya Kamati Kuu ya Chama cha CPC, Mao Dingzhi akiwa ameambatana na Balozi wa China nchini, Chen Mingjian.

Mazungumzo hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam jana Mao Dingzhi pamoja na kumpongeza Dk. Biteko kwa kuteuliwa na kuapishwa kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, alizungumzia kuhusu uhusiano mzuri ulipo kati ya Tanzania na China na kushukuru jinsi Serikali ya Tanzania inavyounga mkono Serikali ya China kwenye majukwaa mbalimbali ya kimataifa. Pamoja na kuzungumzia miradi ya Nishati, Dk. Biteko aligusia maeneo ambayo Tanzania inahitaji ushirikiano kutoka China, ambayo ni pamoja na kujengea uwezo wataalam kwenye masuala ya utawala na teknolojia.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Bureau I na Idara ya Oganaizesheni ya Kamati Kuu ya Chama CPC, Mao Dingzhi alisema Chama cha CPC na Chama Cha Mapinduzi, (CCM), vimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu tangu enzi ya waasisi wa vyama hivyo ambao ni Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Mao Tse Tung na kuongeza kuwa ushirikiano huo unaendelezwa na vyama hivyo hadi sasa. Aidha, alipongeza jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezeshaTanzania kuwa nchi ya amani, uhuru wa kutoa maoni, uzalendo na kuheshimu utu wa wananchi wake na kuahidi kuendeleza ushirikiano kwenye nyanja za uchumi wa kidijitali, masuala ya kijamii, utamaduni pamoja na elimu.

# Tume ya Haki za Binadamu yatia mguu sakala la Pauline Gekul

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, (THBUB), imesema inasudia kufanya uchunguzi wa kina kutokana na tuhuma za ukatili na udhalilishaji unaodaiwa kufanywa na Mbunge wa Babati Mjini, Pauline Philipo Gekul, dhidi ya Hashim Ally Phillemon mkaazi wa Babati Mjini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Makamu Mwenyekiti wa THBUB, Mohaned Khamis Hamad, alisema taarifa za kitendo hicho zimekuwa zikisambaa katika vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii hivyo tume imeamua kufuatilia kwa kina ili kupata usahihi wa taarifa hizo. Alisema pamoja na hatua zilizochukuliwa na mamlaka mbalimbali, THBUB imeona kuna haja ya kufanya uchunguzi huo kwa mujibu wa ibara ya 130 (1) (c) na (f) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 1977 na kifungu cha 6 (1) c, f, g pamoja na kifungu cha 15 (1) (a) vya Sheria ya THBUB, Sura ya 391 ili kubaini ukweli wa tuhuma hizo.

Aidha, alisema Hashim Ally Phillemon alikamatwa na kujeruhiwa sehemu mbalimbali katika mwili wake akiwa mazingira ya kazini kwake jambo ambalo limepelekea kupata maumivu makali katika mwili wake.

"Kama inavyoelezwa na vyombo vya habari kwamba Hashim Ally Phillemon alikamatwa, kupigwa, kujeruhiwa na kuwekewa chupa katika eneo la haja kubwa akiwa kazini kama mtumishi wa Paleii Lake View Garden, inayodaiwa kumilikiwa na mbunge huyo," alisema Makamu Mwenyekiti.

Hata hivyo ameeleza chanzo cha udhalilishaji huo kinadaiwa kuwa ni kutumwa na mshindani wa kibiahara wa mbunge huyo kumuwekea sumu na kumuua. Tuhuma hizo ziliibuka Novemba 25, 2023 baada ya kusambaa kwa video mitandaoni ikimuonesha Hashim Ally Phillemon akielezea ukatili na udhalilishaji aliofanyiwa na mbunge huyo.



# Watumishi sita washikiliwa kwa tuhuma za wizi wa vifaa tiba

**Na Godfrey Sanga**

WATUMISHI sita wa Kituo cha Afya Njombe, wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma za wizi wa vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 15.

Miongoni mwa vifaa vilivyotajwa kuibiwa ni mashine ya kupimia mkojo, mashine ya uchunguzi wa wingi wa damu na vifaa vyake pamoja na vipimo vya Virusi vya Ukimwi.

Hatua hiyo, inakuja baada ya agizo la Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka mara baada ya kufanya ziara katika kituo hicho akiongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa kubaini wizi huo baada ya kuhoji na kusikiliza malezo ya namna vifaa hivyo vilivyoibiwa.

Akizungumza kwa njia ya simu na mwandishi wa gazeti hili, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Hassan Banga, alithibitisha watumishi hao kushikiliwa kwa ajili ya mahojiano kuhusu tuhuma zinazowakabili na kuongeza kuwa uchunguzi utakapokamilika hatua zinazofuata za kisheria zitafuatwa.

Hivi karibuni, watu watumishi wanne wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Njombe, walikamatwa na kusimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi kwa tuhuma zinazowakabili kwa wizi wa seti 15 za televisheni zenye thamani zaidi ya Sh. milioni 11.7 na komputa mbili za hospitali hiyo.

# Wanaosubiri madawati, watasubiri wakiwa nje



**Na Hellen Mwango**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mohamed Mchengerwa, amesema Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Mikoa na Watendaji wengine wanaosubiri Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kupeleka madawati 100 au 50 kwenye maeneo yao, watasubiri wakiwa nje ya mfumo.

Pia, alisema Rais Samia hana baya, alishamaliza kazi yake ikiwamo kuboresha majengo yenye madarasa ya kutosha, watendaji wanaposhindwa kununua madawati 50 wakidai wanasubiri bajeti ya Serikali Kuu, Taifa haliwezi kupiga hatua.

Waziri Mchengerwa alitoa kauli hiyo wakati akikabidhi gari aina ya 'Min bus' kwa ajili ya kuwahudumia watumishi wa Makao Mkuu ya Tume ya Utumishi wa Walimu, kompyuta mpakato 159, pikipiki 62 na kufanya idadi yake kufikia 143 zilizogharimu zaidi ya Sh milioni 800 kupitia fedha za Boost kwa ajili ya kuiongezea tume hiyo ufanisi wa kazi.

"Wale watendaji wanaosubiri bajeti ya Serikali Kuu kununua madawati kati ya 50 hadi 100, nawatangazia kwamba mtasubiri mkiwa nje ya mfumo, hatuwezi kupiga hatua kama tunaongoza kigoigoi, Rais Samia alishamaliza, alishatoa maelekezo katika halmashauri zote, asilimia 70 ya mapato zifanye matumizi na asilimia 30 pia alishaelekeza kazi yake.

"Namshukuru Rais kwa kuingia katika mioyo ya Watanzania, alichagua kushuka kwa wananchi wake kwa kuimarisha ujenzi wa miundombinu, kuweka madawati katika shule zetu, ni jambo la ajabu kuona picha mitandaoni zikionyesha wanafunzi wanakaa chini kwa sababu ya kukosa madawati 50, mkurugenzi unafanya nini, tujitathimini," alisema.

Akifafanua zaidi alisema Wakurugenzi wa Halmashauri nchi nzima, mipango ya maendeleo iendane na mahitaji halisi na wakati kwa wananchi katika eneo husika.

"Shule inahitaji madawati 50, mkurugenzi anasema anasubiri bajeti ya Serikali Kuu, hizi kauli zinamsikitisha sana Rais Samia, hatuwezi kufanyakazi na mtu wa aina hii asiyewajali wananchi na mahitaji yao," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mchengerwa aliielekeza Tume ya Utumishi wa Walimu kwenda kufanya mapitio ya madaraja ya walimu ikiwamo kupata na kutatua changamoto zote ili walimu wafanye kazi kwa ari moja.

Alisema Tume ikishafanya mapitio watakaa pamoja na Rais waone namna moja ya kuwasaidia walimu ili kuendelea kupambana na umasikini.

Kuhusu ujenzi wa nyumba za walimu, Waziri Mchengerwa alisema serikali ilikuwa inamaliza changamoto ya ujenzi wa shule na kuongeza madarasa, lakini sasa inafanya mkakati wa ujenzi wa nyumba za walimu katika maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi.

Alisema walimu wana haki ya kufanyakazi wakiwa wanatabasamu bila kuwa na changamoto yoyote na kwamba kwa serikali hilo litafanikiwa.

Aidha alisema wizara yake ilishatoa maelekezo kwa watendaji wa halmashauri ikiwataka kukamilisha miradi ya shule Novemba 30, mwaka huu na kwa shule maalumu hadi Desemba 30, mwaka huu.

Alisema atafanya ukaguzi kuona iwapo maelekezo hayo yametekelezwa.

Naye Katibu Mkuu wa Tume hiyo, Paulina Nkwama, alisema sunami ya walimu kupanda madaraja ilitokea wakati wa uongozi wa Rais Samia na Waziri Mchengerwa akiwa Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma utawala bora.

Alisema bado anaendelea kuwapambania kwa kuondoa kero ya usafiri kwa watumishi wa tume.

"Rais Samia alifungua milango kwa wadau wa maendeleo na kupitia Boost tumepata kompyuta mpakato, pikipiki na gari la watumishi wa makao makuu, tunamuombea sana Rais wetu," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Elimu),Charles Msonde alisema tume hiyo inaongeza utulivu kwa walimu kwa kushughulikia changamoto ya muda mrefu ikiwamo ucheleweshwaji wa kupanda madaraja.

Alisema serikali kwa kushirikiana na walimu waliweka mkakati wa kuboresha elimu ya sekondari kwa kuanza na twisheni kwa kidato cha kwanza wamefanikiwa kwa asilimia kubwa.

Alisema shule za serikali zote nchini kwa sasa mwanafunzi wa kidato cha kwanza wa mwaka huu anaongea na kuandika kwa lugha ya Kiingereza vizuri kuliko wa kidato cha pili kutokana na kuwajengea uwezo mkubwa walipoanza masomo Januari.

Alisema mbali na sekondari, shule ya msingi wanafunzi wa darasa la tatu wamefundishwa namna ya kuanza kujieleza hayo yote ni kwa sababu walimu wanafanya kazi wakiwa na tabasamu.

# 'Mafunzo Akili Bandia ni muhimu'

**Na Imani Mtumwa, Maelezo - Zanzibar**

MKUU wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Dk. Mahmoud Alawi, amesema mafunzo ya akili bandia ni muhimu kupatiwa wafanyakazi nchini ili kuendeleza mapinduzi ya nne ya viwanda.

Dk. Alawi alitoa rai hiyo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wa taasisi mbalimbali juu ya teknolojia hiyo katika ukumbi wa Taasisi ya Karume Mbweni alisema kwasasa dunia inaelekea kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda ambapo matumizi ya roboti yatahitajika ili kurahisisha utendaji kazi.

Alisema Mafunzo hayo yanaenda kuwajengea uwezo wafanyakazi hao kuweza kutumia roboti katika kurahisisha kazi zao.

Alisema akili bandia (roboti) ina uwezo wa kufanya kazi nyingi kama binadamu hivyo teknolojia hiyo itaenda kuisaidia Serikali hasa katika sekta ya viwanda kutekeleza majukumu yake kwa urahisi zaidi.

Aidha, aliwataka washiriki hao kuwa watulivu na kufuatilia mafunzo hayo ili kufikia malengo yaliokusudiwa.

Kwa upande wake, Naibu Mkuu wa Taasisi Karume Taaluma, Dk. Khamis Khalid Said, alisema kukamilika kwa mafunzo hayo kutasaidia kurahisisha utendaji katika maeneo mbali mbali ikiwemo ya biashara, sekta ya afya, usafirishaji na nishati.

Alisema mafunzo hayo yanafanyika kutokana na mashirikiano mazuri yaliopo kati ya Taasisi ya karume na Chuo cha AP cha Belgium kwa lengo la kupata ubunifu na kuboresha utendaji kazi.

Mkufunzi kutoka Chuo cha AP University, Piric Ven Muoek, alisema katika kuhakiksha mradi huo unafikia malengo wanafunzi wanne wa chuo hicho watapata fursa ya kuendeleza Mafunzo hayo nchini Belgium ili kuweza kuiendeleza programu hiyo Zanzibar.

Naye Mkuu wa programu za uwezeshaji, Wakala wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi (ZEEA), Raya Idrisa Ahmada, alisema mafunzo hayo yanaweza kuleta mabadiliko ya kiutendaji nchini na kuziomba taasisi zinazohusika na masuala ya viwanda kutoa ushirikiano ili kuuendeleza mradi huo hadi kufikia malengo.

Mafunzo hayo ya siku tano yaliwashirikisha wajasiriamali na watendaji wa taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

# Hakimu ataka tathimini

**Na Mwandishi Maalum, Mahakama**

HAKIMU Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Simiyu, Martha Mahumbuga, amewataka watumishi wa mahakama mkoani humo wakiwamo mahakimu kuwa na tabia ya kusimamia, kufuatilia na kutathmini majukumu yote wanayoyapanga.

Alitoa rai hiyo wakati akiongoza kikao cha Menejimenti Mkoa wa Simiyu kutathmini utendaji kazi na kuweka mikakati ya namna ya kufunga mashauri ya mirathi.

Alisema jambo jingine ni kuwa na ubunifu na ushikiriano katika kazi ili kufikia lengo la Mahakama katika kutoa haki na huduma bora kwa wananchi.

"Kila mmoja wetu hapa anatakiwa kujitathmini, tuchukue mawazo baina yetu na kushirikiana," alisema Hakimu Mahumbuga.

Aidha katika kikao hicho, Mahakimu Wafawidhi wa Mahakama ya Wilaya za mkoa huo, waliwasilisha taarifa ya hali ya mashauri, yakiwamo ya mirathi katika kipindi cha mwezi mmoja toka kufanyika kwa kikao cha menejimenti cha mwezi uliopita.

Taarifa hizo zinaonesha kuwa Mahakama za Mwanzo zilizopo ndani ya Mkoa wa Simiyu zimefanikiwa kufunga mashauri ya mirathi kwa asilimia 50 kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Oktoba 27 hadi Novemba 24, mwaka huu.

Hatua hiyo, inafikiwa baada ya kuweka mkakati wa namna ya kufunga mashauri ya mirathi, mahakimu sasa wamejipanga kwenda kumaliza yaliyobaki kwa kutumia mbinu na uzoefu walioupata kutoka kikao hicho.

Naye Mtendaji wa Mahakama Mkoa wa Simiyu, Gasto Kanyairita, aliwasisitiza Mahakimu, Maafisa Utumishi na Maafisa Tawala kuhakikisha wanadhibiti na kufufua maeneo na mipaka ya mahakama na kuwapa notisi taasisi au watu wanaotumia majengo ya mahakama bila vibali.

Pia, aliwashauri kuyafanyia ukarabati wa majengo ya mahakama yaliyochakaa na ujenzi wa vyoo katika Mahakama za Mwanzo zilizopo Mkoa wa Simiyu.

Mtendaji aliwaelekeza Maafisa Utumishi na Maafisa Tawala kuwasisitiza watumishi kuwa na desturi ya kujua afya zao lakini pia kutoa elimu kwa watumishi ili kujua umuhimu wa kupima afya.

"Mjipange na kujiandaa kwa ajili ya wiki ya sheria nchini kwa mwaka 2024 ambayo ina kauli mbiu inayosema, 'Umuhimu wa dhana ya haki kwa ustawi wa taifa: Nafasi ya Mahakama na wadau katika kuboresha mfumo jumuishi wa haki jinai," alisema.

# Mashirika, taasisi 19 zakalia 'kuti kavu'

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inakusudia kuzifutilia mbali taasisi 19 za umma ambazo zimekuwa zikijiendesha kwa hasara.

Msajili wa Hazina, Nehemiah Msechu, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wahariri na waandishi wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana.

Bila kuzitaja taasisi hizo, Msechu alisema tayari mchakato umekwishafanyika wa kuziainisha taasisi hizo na kwamba taarifa zaidi zitatolewa na Waziri mwenye dhamana mwanzoni mwa Desemba, mwaka huu, atakapokutana na waandishi wa habari.

Hatua hiyo inakuja tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aridhie mapendezo ya kufanya mageuzi makubwa katika mashirika na taasisi za umma ili kuongeza ufanisi na kuchangia katika kukuza uchumi wa Taifa.

Rais Dk.Samia aliyasema hayo jijini Arusha Agosti 19, mwaka huu ambapo alifafanua kuwa alipokea

mapendekezo ya kufanya mabadiliko makubwa katika taasisi za umma ambazo kiutendaji zinasimamiwa na Ofisi ya Msajili na kuitaka Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Ofisi ya Msajili wa Hazina, kukutana na wadau kabla ya kuanza kutekelezwa kwa mapendekezo hayo.

Mapendekezo yaliyoidhinishwa na Rais Samia ni pamoja na kufuta baadhi ya mashirika, kuunganisha baadhi ya mashirika na kuanzisha mashirika mapya.

Hata hivyo, Rais Dk. Samia alisema mabadiliko yanayopendekezwa hayalengi kufuta ajira, bali kuboresha utendaji kazi wa mashirika ya umma na hivyo kupunguza mzigo kwa serikali.




Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, akizungumza na wahariri na waandishi (hawapo pichani), kwenye kikao kazi jijini Dar es Salaam jana.



# Samia kuongoza vikao CC, NEC

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, leo anatarajiwa kuongoza kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Halmashauri Kuu CCM Taifa (NEC).

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, alisema juzi kuwa vikao hivyo vitafanyika jijini Dar es Salaam.

Vikao hivyo, vilitanguliwa na vikao vya kawaida vya uongozi ngazi ya Taifa vilivyofanyika Novemba 27 hadi jana.

Katika hatua nyingine, Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, jana alifungua mafunzo (semina) ya wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

Katika semina hiyo, wajumbe walifundishwa mada tofauti zinazohusu uongozi na maadili ili kuongeza uwezo na ufanisi kwa viongozi kuwajibika kwa chama na serikali.

# Mfuko wa Uwekezaji sasa mbioni kuanzishwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI iko mbioni kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Fund – PIF) ambao utawezesha upatikanaji wa mitaji kwa wakati kwa mashirika ya umma.

Hayo yalisemwa na Msajili waa Hazina, Nehemiah Mchechu, katika kikao kazi na wahariri na waandishi wa habari kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana.

Mchechu alisema Sheria ya Mamlaka na majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura 370 haibainishi vyanzo vya fedha za mitaji kwa ajili ya uwekezaji katika taasisi na maeneo mengine.

Alisema vyanzo vya fedha za Mfuko, vitakuwa ni pamoja na sehemu ya maduhuli yatakayokusanywa na Mamlaka ambayo kiwango chake kitabainishwa kwenye kanuni.

Kadhalika, alisema Mfuko utakuwa chini ya uangalizi wa Kamati ya Uongozi ya Mfuko wa Uwekezaji wa Umma.

Mchechu aliongeza kuwa kutakuwa na miongozo itakayoainisha vigezo vya uwekezaji, ufuatiliaji pamoja na mambo mengine yanayohusu uendeshaji wa Mfuko.

Pia alisema kutafanyika mapitio ya utendaji kazi wa kifedha wa mashirika ya umma kwa lengo la kubaini mahitaji na kupendekeza kwa Kamati ya uongozi njia bora za uwezeshaji wa kifedha; kuweka vigezo vya mashirika ya umma kupata fedha za uwekezaji kutoka katika Mfuko; kuidhinisha maombi ya shirika la umma ya kununua hisa; kuwekeza au kuondosha uwekezaji katika mashirika ya umma au maeneo mengine yenye fursa za kibiashara; kusimamia fedha za uwekezaji za mashirika ya umma na kufuatilia na kuhakikisha michango ya mashirika ya umma na gawio kutoka katika mashirika ya umma na kampuni ambazo serikali inamiliki hisa, vinalipwa kwa wakati.

Vile vile, kufuatilia utendaji wa mashirika ya umma kwa madhumuni ya kutathmini uendelevu wake na kupendekeza hatua stahiki ikiwemo kuunganisha au kufuta mashirika husika au kuboresha utendaji.

## Tendo la ndoa, manyanyaso yavunja ndoa Mbeya

**Na Zawadi Kapambwe, Mbeya**

MAHAKAMA ya Mwanzo Mjini imevunja ndoa baina ya Elizabeth Malongo (41) na Asangalwisye Mwamakua (52) wote wakazi wa Uyole, jijini mbeya.

Hakimu wa mahakama hiyo, Nitike Kiputa, alisema baada ya kusikiliza kwa kina pande zote mbili alibaini kuwa ndoa hiyo kamwe haiwezi kurekebishika tena baina yao.

"Ndoa inaunganishwa na watu wawili yaani mke na mume, kadhalika ndo hiyo hiyo inavunjwa na watu hao hao yaani mke na mume," alisema.

Awali ilidaiwa kuwa mdai Elizabeth alifika makakamani hapo kudai talaka kwa madai kuwa hajapatiwa tendo la ndoa kwa muda mrefu pia mume wake na amekuwa akimnyanyasa kila kukicha.

Alisema mbali na kutopewa tendo la ndoa ametelekezwa na watoto kwa kutopewa huduma za matunzo kama chakula maradhi na ada za watoto.

Hata hivyo, hakimu Kiputa alivunjilia mbali ndoa hiyo yenye familia ya watoto sita na kuwaambia kwamba kila mtu yupo huru kuoa au kuolewa na kumtaka mdaiwa kuhudumia watoto kwa chakula, maradhi na elimu.

### MAPUNGUFU TANESCO:

# Simu 40,000 zapigwa kwa siku, 12,000 tu zapokelewa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, amekitaka kituo cha huduma kwa mteja (Call Center) cha TANESCO kuandaa mikakati itakayosaidia kufanya wateja wote wanaopiga simu waweze kuhudumiwa.

Naibu Waziri Kapinga alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipotembelea kituo hicho cha huduma kwa mteja ili kujionea utendaji kazi.

Alisema kumekuwa na mapungufu mengi katika shirika hilo huku mojawapo likiwa ni huduma kwa mteja kwani kwa siku zinapigwa simu 40,000 na zinazopokelewa ni simu 12,000 tu jambo ambalo linafikirisha na kupelekea kuangalia namna bora ya kuboresha huduma ili kuhakikisha kila mtanzania anapata huduma hiyo.

"Niwaelekeze Kitengo cha Huduma kwa Mteja – TANESCO, wahakikishe ndani ya muda mfupi waje na mikakati amabayo itawafanya wateja wote waweze kusikilizwa na changamoto zao kutatuliwa kwa wakati," aliagiza.

Aidha ameongeza kuwa changamoto ambazo ni sugu kwenye shirikika hilo zinapaswa kutatuliwa kwa haraka ili kuendana na kasi ya teknolojia iliyopo.



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga (kulia) akizungumza na mmoja wa wafanyakazi Tanesco. Picha Maktaba Yetu.

Alisema changamoto zinaposhindwa kupatiwa suluhu kuna mambo mawili, aidha shirika limeshindwa au waliopewa jukumu hilo wameshindwa, hivyo, itailazimu serikali kutafuta wengine kwani kwa karne hii suala la huduma kwa mteja halipaswi kuwa kikwazo.

Alisema pamoja na kuwa na changamoto ya umeme lakini mteja hapaswi kuwa na mawazo kwa ajili ya kushindwa kusikilizwa changamoto yake kwani mtu anapopata changamoto anapaswa kutatulia kwa muda wa saa tatu mpaka nne.

"Kwa takwimu za sasa hivi asilimia 32 wanahudumiwa kati ya saa tatu mpaka nne lakini asilimia 52 wanahudumiwa ndani ya saa nane niwaambie tu tulipofikia sasa umeme sio anasa, umeme ni suala la msingi kwa kila Mtanzania, huwezi kumuacha mteja saa 12 hana umeme kwa sababu umeshindwa kwenda kumtatulia changamoto yake, mgao ni kitu kingine na kumtatulia mteja changamoto yake ni jambo lingine," alisisitiza.

Pia aliwataka kuhakikisha wanawalipa stahiki zao wafanyakazi wote wa kituo hicho ili waendelee kuto huduma bora na stahiki kwa mteja na amewataka watoa huduma kutambua kuwa mteja ni mfalme hivyo wanapaswa kumuhudumia kwa nidhamu.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Huduma kwa Mteja, Martine Mwambene, alisema wamepokea maelekezo yote na watayafanyia kazi kwa wakati.

"Tumepokea maelekezo na tutayafanyia kazi kwani tayari tumeshaanza kuandaa mitandao mbalimbali ambayo tunaweza kuwasiliana na mteja ikiwemo mitandao ya kijamii lakini pia kwa kutumia SSD CORD," alisema.

## Mtanzania aliyeuawa Israel kuzikwa leo

**Na Mwandishi Wetu**

MWILI wa Mtanzania Clemence Mtenga (22), aliyeuawa nchini Israel, unatariwa kuzikiwa leo nyumbani kwake, huko Kijiji Kirwa Mashati, wilayani Rombo.

Mwili huo ulikabidhiwa kwa familia yake baada ya kuwasili saa 2:51 kwa ndege ya Shirika la KLM kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) ukitokea Israel.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, akizungumza baada ya kuukabidhi mwili kwa familia, alisema mwili huo umeukaguliwa na familia na kuthibitishwa kuwa ndiye kijana wao Clemence.

Bado haijafahamika Mtenga alikufa vipi lakini mwanafunzi huyo wa kilimo mwenye umri wa miaka 22 alifariki wakati wa mashambulizi ya Oktoba 7, mwaka huu, wakati wapiganaji wa Hamas walipoanzisha shambulio ambalo halijawahi kushuhudiwa dhidi ya Israel kutoka Ukanda wa Gaza.

Mtenga alikuwa nchini Israel kama sehemu ya mpango wa masomo, alifika mwezi mmoja tu kabla ya shambulio hilo.

Wiki hii alitunukiwa shahada yake kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha



**Mwili huo umeukaguliwa na familia na kuthibitishwa kuwa ndiye kijana wao Clemence.**

# Baadhi ya maafisa ardhi wadaiwa kuhonga viongozi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amesema baadhi ya watendaji sekta ya ardhi wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakiwahonga baadhi ya viongozi kwa kuwapa viwanja kama kinga yao mara wanapokutwa na makosa ili hali ya viongozi hao wanakuwa hawana taarifa kama watendaji hao wana nia ovu.

Waziri Silaa alisema hayo mara baada ya kufika eneo lenye mgogoro linalomilikiwa na Kanisa la Morovian kiwanja namba 1,2 na 3 Block T, Mtaa wa Itega jijini Dodoma jana.

"Kuna wakati wakurugenzi wa mamlaka za upangaji na watendaji wizarani ambao wamekuwa wakipima viwanja kwa watu wenye nguvu na kuacha kumpimia ardhi ambaye hana nguvu, katika uongozi wangu kama Waziri mwenye dhamana nitaweka mstari uliyonyooka na stashiriki katika dhammbi kama hii," alisema.

Kwa upande mwingine Mchungaji wa Kanisa la Morovian amemshukuru Waziri Silaa na Serikali kwa ujumla kwa kufika eneo la tukio na kutatua mgogoro uliowakabili kwa muda mrefu kwani wameteseka kwa kipindi kirefu na mgogoro huo bila kuwa na mafanikio.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Ajira kwa watoto

SUALA la kuajiri wasichana wa kazi katika umri mdogo limetajwa kukithiri sana katika kipindi cha kuhitimu shule kwa wanafunzi hususani kwa darasa la saba.

Sheria inataja umri wa mtu yeyote kuingia kwenye ajira ni kuanzia umri wa miaka 18, tofauti na hapo ni utumikishwaji na unyanyasaji ambao unatajwa kuwa kinyume cha sheria.

Ushauri wangu kwa wote wanaajiri katika rika hilo ni kuacha haraka sana, haijalishi matokeo yake ni mabaya au hajabahatika kuendelea na shule.

**Sheria inataja umri wa mtu yeyote kuingia kwenye ajira ni kuanzia umri wa miaka 18, tofauti na hapo ni...**




## MAONI YA MHARIRI

# Mashirika yatakayopona kupigwa panga yazinduke

MBALI na kutoa ajira, taasisi za umma zilianzishwa kwa malengo mbalimbali, kubwa ikiwa ni kutoa huduma kwa Watanzania.

Baadhi ya taasisi hizi zilibinafsishwa, lakini nyingine bado zinaendeshwa kwa pesa za umma.

Ni kweli kwamba zipo taasisi za umma ambazo zimekuwa zikifanya vizuri, hadi nyingine kutoa gawio kwa serikali. Hizi ni za kupongezwa sana.

Hata hivyo, kumekuwa na taasisi za umma ambazo zimekuwa mzigo, hivyo kuendelea kuzikumbatia ni kuzidi kuwatwika walipa kodi wa nchi hii mzigo.

Ni katika muktadha huo, serikali sasaimejipanga kufuta taasisi 19 za umma ambazo zimekuwa zikijiendesha kwa hasara.

Kwa mujibu wa Msajili wa Hazina, Nehemiah Msechu, tayari mchakato umekwishafanyika wa kuziainisha taasisi hizo ambazo bado hazijatajwa majina.

Hatua hiyo inakuja tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aridhie mapendezo ya kufanya mageuzi makubwa katika mashirika na taasisi za umma ili kuongeza ufanisi na kuchangia katika kukuza uchumi wa Taifa.

Mapendekezo yaliyofikishwa kwa Rais Samia ni pamoja na kufuta baadhi ya mashirika ya umma, kuyaunganisha na kuanzisha mashirika mapya pale itakapoonekana inafaa.

Tunashukuru kauli ya Rais Samia kwamba mabadiliko yanayopendekezwa hayalengi kufuta ajira, bali kuboresha utendaji kazi wa mashirika ya umma na hivyo kupunguza mzigo kwa serikali.

Tunaunga mkono hatua hii ya serikali kwani ina nia njema ya kupunguza mzigo kwa walipa kodi na mashirika yatakayounganishwa kuchochea ufanisi.

Tunaamini hatua hii itasaidia pia kuwaamsha watendaji wa mashirika mengine yanayolegalega kuongeza juhudi na ubunifu katika kuhakikisha mashirika yao hayajiendeshi kwa hasara au kutotoa tija kubwa kwa umma.

Ni ukweli kwamba baadhi ya watendaji wa taasisi za umma wamekalia ubadhirifu na matumizi mabaya ya raslimali fedha kulinganisha na jinsi wanavyopambana katika kuhakikisha mashirika yao hayajiendeshi kwa faida.

Unakuta taasisi ya umma kila mara watu wanaendesha semina na safari za kulipana posho kubwakubwa na hivyo kusababisha kila mwaka bajeti ya mshirika hayo kuwa na nakisi inayobebwa na serikali.

Katika hali hiyo hakuna sababu ya kuendelea na taasisi kama hizi ambazo ni mzigo.

## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com




# Kila mmoja apinge ukatili wa kijinsia

UKATILI wa kijinsia ni kitendo chochote ambacho kinaweza kusababisha madhara ya mwili, kingono au kisaikolojia au mateso kwa wanajamii, ikiwa ni pamoja na kutishiwa maisha, kunyimwa uhuru, iwe hadharani au kwa kificho.

Ukatili wa kijinsia hufanywa na hutokea katika nyanja tofautitofauti moja wao ni kupitia mitandao.

Ukatili wa kijinsia kupitia mitandao haujajulikana vema kwa watu wengi lakini upo na umesababisha madhara makubwa.

Ukatili huu huwakuta zaidi vijana wanaotumia vyombo vya habari vinavyohusisha mawasiliano ya kimtandao. Ukatili wa kijinsia kwa njia ya mitandao unapotekelezwa husababisha athari nyingi hasa za kisaikolojia.

Mtu anayetendewa ukatili huu huwa na hofu, wasiwasi, hukosa amani na furaha na pia husononeka na kukosa kujiamini.

Pili ni ukatili wa kijinsia mitaani. Huu unahusisha uchokozi kwa wanawake na wasichana mitaani ni ukatili wa kijinsia. Mara nyingi wanawake na wasichana hudhalilishwa, huogopeshwa na hivyo hukosa kujiamini wawapo mitaani. Kumbuka kila mtu ana haki ya kuwa huru mahali popote bila ya kubughudhiwa.

Tatu ni vishawishi na ulaghai. Wakati mwingine vishawishi kwa watoto wa kike ni ukatili wa kijinsia. Umbali wa kwenda shuleni kwa wanafunzi ni tatizo kubwa, hasa kwa watoto wa kike. Baadhi ya watoto hujikuta katika ushawishi na ulaghai unaofanywa na watu mbalimbali wakiwemo waendesha bodaboda, hali inayosababisha kukata tamaa na kukatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupata mimba na kuolewa katika umri mdogo.

Ukatili mwingine kwa watoto ni utumikishwaji wa watoto. Huu pia ni ukatili wa kijinsia pia. Utumikishwaji wa watoto huwakosesha watoto haki zao za msingi, pia huwaathiri kisaikolojia na kimwili.

Kukosa haki ya kuwa kiongozi kwa ajili ya tu ya jinsi ya mtu pia ni ukatili wa kijinsia. Hakuna asiyefahamu kuwa uongozi ni haki ya kila mtu bila kujali jinsia. Maamuzi shirikishi yanayozingatia jinsia zote huleta amani, usawa na maendeleo kwa wote katika jamii.

Kutelekeza familia ni ukatili mwingine wa kijinsia. Tabia hii husababisha chuki, maradhi na watoto kukosa haki zao za msingi. Muhimu kujua kuwa jukumu la malezi ya watoto ni la wazazi wote.

Pia ukeketaji ni ukatili mwingine wanaofanyia wasichana na wanawake. Ukeketaji ni kitendo cha kuondoa au kukata sehemu sisi za mwanamke bila sababu za kiafya.

Ukeketaji husababisha maumivu makali ya kidonda, kutokwa na damu nyingi, kuzimia, maumivu ya kisaikolojia, kuziba kwa njia ya mkojo na kuchanika vibaya wakati wa kujifungua.

Lakini pia ukeketaji husababisha kuchelewa kujifungua na kupata maambukizi ya magonjwa kama VVU, fistula, homa ya manjano na hata kifo. Muhimu zaidi ni kusaidia kuelimisha jamii kuhusu athari za ukeketaji zinazotokana na mila na desturi hatarishi.

Kumpiga mwanamke ni unyanyasaji mwingine wa kijinsia na udhalilishaji. Kipigo husababisha chuki, woga, visasi na uhusiano mbaya ndani ya familia. Mwanaume wa kweli hawezi kumpiga mwanamke. Mwanamke jasiri hutoa taarifa kuhusu vipigo.

Mjamzito ana haki ya kupumzika. Kumpa majukumu mengi mjamzito ni ukatili mwingine wa kijinsia. Kazi ngumu kwa mjamzito huweza kusababisha kuharibika kwa mimba na matatizo mengine ya kiafya. Ni vyema mjamzito apunguziwe majukumu na apewa muda wa kutosha kupumzika. Baba ni muhimu kumsaidia kazi mkewe mjamzito.

Mtoto bila kujali jinsi yake pia ana haki ya kupata elimu. Kumyima elimu mtoto wa kike, japo hili siku hizi limepungua ni ukatili pia wa kijinsia. Hali ya mtoto wa kike kukosa elimu huchangia mimba za utotoni, ndoa za utotoni na ongezeko la unyanyasaji kwa watoto wa kike.

Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inaeleza kwamba ni jukumu la mzazi, mlezi au mtu yeyote anayeishi na mtoto kumpa haki ya elimu na kujifunza.

Mpe mtoto wa kike elimu umkomboe na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

# Katambi asisitiza uzalendo kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu**



NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amewataka vijana nchini kuwa wazalendo na kuzingatia maadili ili kuwa Taifa bora sasa na baadaye.

Akifungua kongamano la vijana la kisayansi jana linalofanyika mkoani Morogoro, Katambi alisema vijana wana mchango mkubwa katika ujenzi wa Taifa.

"Vijana wana mchango mkubwa katika ujenzi wa Taifa na wanaweza kutoa mchango mkubwa zaidi iwapo mtafanya shughuli zenu kwa kuzingatia uzalendo, weledi na maadili," alisema.

Aidha, alisema utafiti wa viashiria vya Ukimwi mwaka 2016/17 nchini, umeonyesha kuwa moja ya makundi yaliyo nyuma katika kufikia malengo ni vijana, huku wengi wenye umri mdogo hawajui hali zao za maambukizi ukilinganisha na watu wenye umri mkubwa, hali inayosababidha vijana wenye virusi vya Ukimwi kutoanza dawa za ARV mapema.

Katambi alitoa rai kwa vijana nchini kujitokeza kwa wingi katika huduma za upimaji wa VVU kwa hiari sambamba na kupiga vita mmomonyoko wa maadili.

# Nipo tayari kupokea talaka lakini mtoto sitamuachia

**Na Zawadi Kapambwe, Mbeya**

MDAIWA katika kesi ya madai ya talaka ameieleza mahakama kuwa yupo tayari kupokea talaka ila kwa sharti la mdai kumuachia watoto.

"Muheshimiwa hakimu huyu, bwana alishatutelekeza muda mrefu mimi na wanangu. Hapo alipo ana mke mwingine na watoto, ameona mke mdogo amemuacha ndio anarudisha mbavu zake kwangu," alisema.

Mdaiwa katika kesi hiyo ya madai ya talaka Mariam David (40) mkazi wa Mabatini jijini hapa alisema migogoro kati yake na mumewe ilianza mara baada mumewe kupata mwanamke mwingine.

Mdai aliendelea kuifafanulia mahakama wakati akiishi na huyo Bibi mdogo, alipata ajali mbaya sana na ndipo huyo Bibi mdogo alipomtimua na kumtupia vitu vyake njee, ndipo aliporudisha miguu yake nyumbani.

"Kiukweli huyu bwana mimi siwezi hata kurudiana naye, hapo alipo hawezi hata kufanya tendo la ndoa ajali aliyopata iliharibu nyonga, sasa kama alivyokuwa mzima aliniona mimi siendani naye na kuamua kuoa hivyo arudi tu kwa mke wake," alisema mdaiwa huyo.

Awali mdai Fredy Edson (43) alifika mahakamani akiomba mahakama kuvunja ndoa yake kwa madai kuwa mkewe amekuwa akimrudia usiku wa manane na wakati mwingine harudi kabisa.

Mdai alitoa madai yake mbele ya Hakimu Nitike Kiputa wa Mahakama ya Mwanzo Mjini.

Hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba11, mwaka huu, itakapotolewa hukumu.

# RC atwisha mzigo Maafisa Tarafa, Watendaji Kata

**Na Mwandishi Wetu, Tabora**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Burian, amewataka Maafisa Tarafa na Watendaji wa Kata kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele kuzuia migogoro kati ya Serikali na wananchi ikiwamo migororo ya ardhi.

Alisema kutokana na migogoro hiyo kuanzia katika ngazi zao za majukumu, wanatakiwa kuwa wa kwanza kuzuia na kuimaliza ili amani iendelee kutawala.

Alisema hayo wakati akifunga mafunzo ya siku mbili kwa viongozi hao yaliyofanyika mkoani humo juzi.

Alisema migogoro ya ardhi ni changamoto kubwa katika maeneo mengi na kuwaelekeza maafisa hao kuwa wazalendo na imani na kutumia misingi ya haki na sio upendeleo pale linapokuja suala la uuzaji wa ardhi za watu.

"Wananchi wanalalamika kutoka baadhi ya vijiji viongozi kuuza ardhi, hii itasababisha baadaye migogoro kati ya Serikali na wananchi wake, mnapaswa kuwa na maadili mnapotekeleza majukumu yenu," alisema Dk. Burian.

Aidha, alisisitiza kwamba viongozi hao kuwa na ushirikiano mzuri na wananchi wanaowaongoza kwenye maeneo yao ili kujenga amani.




# Atupwa jela maisha kwa kubaka binti ya kakake

**Na Mwandishi Wetu, Iringa**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi, mkoani Iringa imemuhukumu Mkude Nziku (20), mkazi wa Kijiji cha Kihanga wilayani Iringa kutumikia kifungo cha maisha jela na kulipa fidia ya Sh. milioni tano baada ya kumkuta na hatia ya kumbaka binti wa kaka yake mwenye umri wa miaka 11.

Kesi hiyo ilisimamiwa na Hakimu Mkazi Mkuu wa mahakama hiyo, Said Mkasiwa, iliyokuwa na jumla ya mashahidi wanne akiwemo binti anayedaiwa kubakwa, mama mzazi wa binti huyo, daktari pamoja na polisi aliyechukuwa maelezo ya awali.

Ilielezwa siku ya tukio mtuhumiwa aliingia chumbani kwa binti huyo kupitia njia ya dirisha akamchukua mtoto huyo kwa nguvu kutoka kitandani akamuweka chini kisha kumvua nguo zake na kutenda unyama huo.

"Alinivua sketi akaivuta nguo yangu ya ndani akaniingiza sehemu ya kukojolea nilihisi maumivu makali nikapiga kelele mama akaja chumbani kwangu lakini Mkude alikimbia," alisema binti huyo.

Nae shahidi wa pili ambaye ni mama mzazi wa mtoto huyo, alisema baada ya kusikia kelele za mwanaye alitoka haraka hadi chumbani kwa mwanaee akapishana na mtu sebuleni alianza kumkimbiza punde mtu huyo aliyemtaja kama Mkude akaanguka chini akammulika taa yake ya sola na kumtambua, akamuuliza ulikuwa unafanya nini chumbani kwa binti yako (Mtoto wa kaka yake) Mkude akadai

# Abiria kuchimba dawa dakika 20

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, (LATRA), imeyataka mabasi ya usafirishaji mikoani kuzingatia muda wa kuchimba dawa kuwa ni dakika 20 badala ya 10.

Mkurugenzi wa LATRA, CPA Habibu Suluo, alitoa agizo hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha juzi.

"Kusimama eneo la huduma kwa walau dakika 20. Mambo ya kuchimba dawa dakika 10 hakuna."

Aliwataka wasafirishaji kutoacha abiria wakati kuchimba dawa, pia wazingatie usafi wa basi ikiwemo kumwagilia dawa za kuua wadudu pia kuweka vifaa vya kuhifadhi taka.

## Dondoo za wiki

Na Mwalimu Paul Masatu
Simu: +255 766 775 255

# Unajua nini kuhusu changamoto maishani?


LEO imenipendeza niorodheshe moja ya tabia mbaya ambayo ni kikwazo kwenye mafanikio yako. Ndugu yangu, kama unayo hii tabia hakikisha unaishughulikia na kuiacha, yaani usiingie nayo tabia tunayoimulika hasa ni ya kukataa tamaa dhidi ya changamoto badala ya kupambana.

Ukiona sasa hivi huna tatizo au changamoto, haina maana kama kweli hakuna matatizo au wala siyo kwamba una bahati mbaya sana, hiyo ni kwamba umezidiwa uzito, wewe ndhaifu kuliko hayo yanayokutokea.

Panapotokea hali kama hii unachotakiwa kufanya, kwanza kwa waja wake.

Kwamba anawapima ili kuona kama watamshukuru au kumkufuru.

Kwa hiyo kunapotokea changamoto kwa mujibu wa mlango huo wa maandiko, kazi



mwaka mpya wa 2024.

Ndiyo, inawezekana kwa sababu kila kitu ni uamuzi. Kama anavyosoma mwandishi wa Safu ya Kliniki ya Fikra katika gazeti hili, watu wenye nguvu ya akili na busara hupenda hufanya mabadiliko chanya kwa maana ya kuwa tayari kubadilika wakishaamini kwamba jambo fulani lina faida kwao kama vile kufanya mazoezi au kudumu na ibada.

Hawa hawaishii kutamani tu moyoni kwamba nitafanya kesho, nitafanya kesho na kesho kuzaa kesho bali hufanya kweli mara moja.

### CHANGAMOTO

Changamoto ni sehemu ya maisha. Moja kati ya mazao ya safari za maisha ni kuzalisha changamoto au matatizo. Na changamoto kwenye maisha yako sasa hivi, ila ni kwamba nguvu yako kimtazamo ni kubwa kuliko matatizo au changamoto zinazotokea sasa hivi kwako.

Kwa maana nyingine, wewe ni mkubwa kuliko matatizo au changamoto zinazokutokea na kukuzunguka. Ukubwa huo wa kimtazamo unakupa nafasi ya kuzishinda changamoto kiurahisi na wakati mwingine hii inatokea tu (in automatic way).

Lakini kwa upande mwingine ukiona unaanza kuhisi unapitia tatizo au changamoto kwenye maisha yako, tafsiri yake ni kuwa, hayo matatizo au changamoto yanayokumabana nayo sasa, yana nguvu kuliko wewe, ndiyo maana unapata hisia za kutatizika na tatizo au changamoto husika.

Kwa hiyo hakuna cha ajabu ni kuwa na utulivu. Kisha anza kupiga hatua mojamoja taratibu kutoka kwenye hali hii ya kuzidiwa na changamoto.

Hatua ya kwanza ni kukubaliana na hali halisi, kama changamoto hiyo ilipata mlango wa kuingilia, basi lazima mlango wa kutokea upo.

Katika hatua hiyo ya kuwa mtulivu, anza kujipanga ukikumbuka kuwa maandiko yanasema "Hiyo ni kawaida kwa wanadamu" na wewe siyo wa kwanza. Watu walishapata tatizo kama hilo na wakatoka, wakatangaza ushindi na wao leo ni mfano wa kuigwa.

Baadhi ya maandiko ya dini yanaonesha kwamba changamoto, matatizo, misiba, magonjwa na majanga mengine ni mitihani ya Mwenyezi Mungu ya mja si kumkufuru Mwenyezi Mungu wala kufanya kutapata na kwenda kufanya ushirikiana bali kuendelea kupambana huku akimtegemea Mwenyezi Mungu kwa kila kitu.

### MTAZAMO WAKO

Hatua ya pili mbayo inapaswa kuwa tabia yako mpya kama huna, ni kila wakati kushughulika na mtazamo wako. Lione tatizo katika picha inayostahili, usilione tatizo kama laana, bahati mbaya. Yaani usijione mnyongem badala yake tengeneza mtazamo wako vizuri.

Lione tu kama sehemu ya maisha. Kwamba limetokea kwa sababu yoyote ile inayoweza kuwa na hivyo ukijipanga vizuri, ukajiimarisha kwenye mtazamo, itakupa nafasi ya kuwa na nguvu zaidi ya hiyo changamoto.

### KUDHIBITI HISIA

Hatua ya tatu ni kudhibiti (control) hisia na mawazo yako. Mara nyingi unapopata tatizo, hisia na mawazo yako vitakulazimisha kuweka mtazamo (focus) kwenye tatizo.

Mawazo yatataka kukupeleka kuwaza hilo tatizo mara kwa mara, hisia zako zitataka uendelee kupata hisia juu ya hilo tatizo. Tafadhali usikubali mwelekeo huo na badala yake, pambana kudhibiti hisia hizo.

Jitahidi kuhamisha jicho lako kutoka kwenye tatizo na tafuta jambo lingine zuri na hivyo anza kutafakari hilo. Kuendelea kulitafakari tatizo hakukusaidii bali unaendelea kumwaga mafuta kwenye moto.

### KUTAFUTA MAARIFA

Hatua nyingine ni kutafuta maarifa au ufahamu utakaokuimarisha zaidi kukabiliana na hiyo changamoto. Maarifa kuhusu changamoto inayokukabili yanapatikana kwa watu wazoefu, wasomi na hata siku hizi mitandao ya kijamii inatusaidia kwa maana ya ku- google ili kupata ufahamu zaidi. Lakini zingatia kila wakati kwamba siyo kila kinachopatikana kwenye 'Profesa Google' ni sahihi na cha kufanyia kazi!

**Lakini kwa upande mwingine ukiona unaanza kuhisi unapitia tatizo au changamoto kwenye maisha yako, tafsiri yake ni kuwa, hayo matatizo au changamoto yanayokumabana nayo sasa, yana nguvu kuliko wewe, ndiyo maana unapata hisia za kutatizika na tatizo au changamoto husika.**

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA | Jumatano Novemba 29 - Desemba 5, 2023 |

# Jungu kuu






# Wanaowapa mimba wanafunzi stahiki yao ni jela

UK. 12 & 13

Elimu



# Bodi za shule zihamasishe wazazi, wadau kuchangia chakula shuleni

**Na Reubeni Lumbagala**

BODI za shule za sekondari na kamati za shule za msingi ni vyombo maalumu vilivyopo kisheria katika sekta ya elimu kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza maendeleo ya elimu katika shule husika.

Uongozi wa wajumbe wote wa bodi na kamati za shule hupatikana kwa kuzingatia sifa maalumu zilizoainishwa.

Bodi na kamati za shule hushirikiana na uongozi mzima wa shule, serikali na wananchi katika kusimamia maendeleo ya shule. Hata inapokuja mipango na masuala ya kimaendeleo ya shule kama vile ujenzi wa miundombinu, uchangiaji wa chakula shuleni, nidhamu ya wanafunzi shuleni, bodi na kamati za shule hushirikishwa kikamilifu kama wadau wakubwa na muhimi wa maendeleo ya shule.

Moja ya changamoto kubwa katika shule za sekondari na msingi za kutwa ni ukosefu wa chakula shuleni.

Wanafunzi kukosa chakula shuleni inachangia sana utoro na ufaulu duni wa wanafunzi.

Mwanafunzi mwenye njaa hawezi kuelewa kinachofundishwa na mwalimu wake darasani na kama haelewi kinachofundishwa ni dhahiri kwamba hawezi kufaulu vizuri masomo yake.

Watalaamu wa lishe pia wanatuambia vyakula vina virutubisho muhimu ikiwemo vitamin D na B, madini ya chuma na selenium, vitu vinavyosaidia kujenga na kuimarisha afya ya ubongo na kumwezesha mwanafunzi kuwa na kumbukumbu sahihi ya mambo anayosoma.

Hivyo suala la wanafunzi kupata chakula au uji shuleni ni suala muhimu ambalo halihitaji kuwa na elimu ya chuo kikuu kufahamu umuhimu wake.

Mwezi Januari 2016, serikali ya Awamu ya Tano ilianza utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo kuanzia shule za awali hadi kidato cha nne.

Kwa kutambua umuhimu wa elimu na hali za kiuchumi za Watanzania, serikali iliona ni busara kuanza kugharamia ada na michango mingine muhimu ya elimu ili wazazi na walezi wapunguziwe mzigo mkubwa wa kusomesha watoto.

Lakini kumekuwepo na dhana potofu kwa baadhi ya Watanzania ambao kwa makusudi au kwa kutoielewa vizuri sera ya elimu bila malipo, husema kuwa wazazi na walezi hawatakiwi kuchangia chochote katika sekta ya elimu kwa kuwa elimu ni bure na serikali ndio inahusika kufanya kila kitu katika elimu. Hii si sahihi hata kidogo.

Pia wazazi wengi wanaamini mwanafunzi kurudi nyumbani kula ndiyo rahisi bila kuzingatia muda ambao mtoto anakaa na njaa akiwa shuleni na madhara yake kielimu.

Mbaya zaidi baadhi ya wanafunzi wanaishi mbali na shule. Hii pia imechangia baadhi ya wanafunzi, hususani wasichana kurubuniwa kupitia chakula na 'mafataki' na kujikuta wamepata ujauzito na kukatisha ndoto zao.

Ripoti ya hivi karibuni ya Utafiti wa Afya Mtoto na Viashiririia vya Malaria ya mwaka 2022 ilionesha kwamba mkoa wa Songwe unaoongoza kitaifa kwa kuwa na idadi kubwa ya wenye mimba za utotoni.

Takwimu zilionyesha kwamba kwa kila wasichana 100, wasicha karibu nusu ya hao, yaani wasichana 45 hupata mimba za utotoni mkoani Songwe!

Mikoa inayofuata kwa uwingi wa mimba za utotoni ni Ruvuma wenye asilimia 37, Mkoa wa Katavi asilimia 34, Mara asilimia 31 na Mkoa wa Rukwa wenye asilimia 30.

Kwanza ieleweke kuwa hakuna elimu bure mahali popote duniani. Elimu inagharimu fedha nyingi sana katika uendeshaji wake. Elimu inahitaji fedha za kuwalipa walimu na watumishi wasio walimu, kujenga madarasa, mabweni, vyoo, maktaba, maabara, ofisi, majiko, kununua vitabu, chaki, karatasi, chakula, kalamu, vifaa vya maabara, kulipia huduma za umeme, maji safi nk.

Haya ni baadhi tu ya mahitaji muhimu ya elimu popote duniani na Tanzania ikiwemo. Kilichofanywa na serikali ni kuchukua jukumu la kugharamia elimu katika mambo ya msingi zaidi lakini baadhi ya masuala kama mavazi ya wanafunzi na kula chakula shuleni bado ni wajibu wa wazazi.

Naamini hadi hapa ndugu msomaji wa makala hii umeshapata picha kuhusu gharama kubwa za kuendesha elimu. Hivyo kudhani kuwa wazazi na walezi hawatakiwi kuchangia chochote katika elimu ni suala ambalo litachelewesha sana maendeleo ya sekta hii muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Kutokana na umuhimu wa chakula shuleni kama nilivyokwishaeleza, upo umuhimu mkubwa kwa wajumbe wa bodi za shule za sekondari na kamati za shule kwa shule za msingi, kuhamasisha wazazi, walezi na wananchi kwa ujumla kuchangia chakula ili watoto waweze kusoma wakiwa wameshiba.

Wajumbe wengi wa bodi na kamati za shule ni wakazi wa sehemu ambazo shule zimejengwa na wengi wanao watoto wanaosoma katika shule hizo. Wajumbe wengi wa bodi na kamati za shule wanauelewa mkubwa wa elimu, hivyo suala la kuchangia chakula ili watoto wao waweze kula shuleni ni suala ambalo kwao halina tatizo kubwa sana kwa sababu ya uelewa wao.

Kutokana na umuhimu wa chakula shuleni, serikali za mitaa na vijiji zinaweza pia kusaidia kwa kutunga sheria ndogo za kuwabana wazazi kutoa ushirikiano.

Ni muhimu sana bodi au kamati hizi kuita kikao cha wazazi, wazee maarufu pamoja na uongozi wa kijiji au mtaa husika kukutana katika eneo la shule na kutoa elimu kwa wazazi juu ya umuhimu wa chakula na kuwaelimisha kwamba chakula ambacho mwanafunzi atakula shule ni kilekile ambacho angekula akiwa nyumbani kwa mchana na hata jioni kwa zile shule ambazo wanafunzi wanalala shule.

Pia kuwafafanulia madhara ya kutokula chakula cha kwa muda mwafaka kuwa ni pamoja na kupatwa na ugonjwa wa vidonda vya tumbo, kuchelewa kwa baadhi ya vipindi kwa wale ambao watarudi kwenda kula nyumbani kama watakuwa wanaishi mbali na shule.

Bodi na kamati pia zinapaswa kushirikiana na walimu, wanafunzi na wazazi katika kuanzisha bustani na mashamba ya chakula, kuhamasisha upandaji miti ya matunda, kuongea na wadau kuchangia chakula lakini kubwa ni kuendelea kuwahamasisha wazazi kuchangia chakula.

Natoa rai kwa bodi na kamati za shule kote nchini kutolala usingizi katika hili kwani wanaweza hata kutembelea shule ambazo zamani zilikuwa hazitoi chakula lakini sasa zinatoa waone jinsi ufaulu ulivyoongezeka huku utoro ukipungua sana.

Itapendeza kuona tunapoingia mwaka 2024, shule zote za kutwa nchini ziwe zinatoa chakula kwa wanafunzi. Kimsingi wazazi wengi kama si wote wanaweza kuchangia na kinachotakiwa ni uelewa tu.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma. Mawasiliano yake ni 0620-800462.

Kolamu



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Malezi aina hii huchangia watoto kuharibika



HIVI karibuni, wakati ninatoka kufanya ibada msikitini, niliandamana na bwana mmoja wa mtaani kwetu, akaniambia amefurahi kusikia moja ya nyumba pale uswahilini kwetu inauzwa.

Akasema anatamani nyumba za urithi ambazo alidai kwa sasa wanaishi wajukuu ziendelee kuuzwa ikiwemo ambayo siku hizi kila wikiendi kunapigwa mnanda na kuondoa utulivu mtaani kwetu.

Kwa nini anafurahia? Alisema amegundua nyumba za urithi ndizo zenye watoto wengi vibaka, wanaokataa shule, wanaokwenda kwenye mabaya usiku kujiuza na kushiriki maovu mengine mtaani kwetu.

Nikaungana naye kutamani nyumba kunakopigwa mnanda au sijui ndio mnaita muziki wa singeli, iuzwe kwani ni kero.

Mbali na kuondoa utulivu kwa watoto, wanafunzi na wagonjwa, mnanda huvutia pia vijana 'wabaya'.

Siku moja niliambiwa malalamiko juu ya mnanda yalishawafikia wakubwa wa mtaa wetu, Temeke Maganga lakini 'wakapotezea' kwa madai hao ni wapiga kura wao!

Yule muumini mwenzangu akanigeukia tena: "Unajua ile nyumba jirani yako ambayo tunahisi inafuga vibaka ni ya urithi pia. Hata ile nyingine wanapouza miguu, vichwa na utumbo wa kuku ni ya urithi. Nasikia pombe haramu zinauzwa pia hapo na humo ndani ni danguro."

Katika uchunguzi wangu mdogo nilioufanya nimegundua kwamba anachokilalamikia huyo muumini mwenzangu ni malezi mabaya tu. Na si kweli kwamba kila nyumba ya urithi ina shida bali hata zisizo za urithi.

Kwanza ni kweli kwamba pale uswahilini kwetu hali si shwari sana muda wote. Ukiacha hilo eneo kunakopigwa mnanda, kuna eneo vijana wenye macho mekundu wanacheza kamari toka asubuhi hadi jioni. Ni ukweli pia kwamba yapo matukio ya wizi usiku na uporaji, hususani simu.

Hapo nyuma, wakazi wa mtaa wetu, tulikaa kikao na kupitisha mchango ili kuziba baadhi ya vichochoro kwa lengo la kukabiliana na wimbi la wizi na wacheza kamari lakini, ni kama tuliochangia mifuko ya simenti tumepoteza pesa bure!

Wiki iliyopita yalipotoka matokeo ya darasa la saba, nikatajiwa orodha ndeefu ya watoto wa mtaani kwetu ambao ambao pia tungesikia matokeo yao ya kuhitimu darasa la saba lakini walishakataa shule kitambo!

Katika orodha hiyo, idadi kubwa ilikuwa ya wale waliokataa shule wakiwa kidato cha pili na cha tatu. Lakini damu ilininisisimka kuambiwa kwamba miongoni mwa hao yumo mvulana aliyeamua kuwa shoga!

Kwa hiyo mtaani kwetu, suala la mtoto kukataa shule na wazazi au walezi wakamwangalia tu ni la kawaida.

Nikawaida pia kuona toka asubuhi hadi usiku vijana wa mtaani kwetu wamekaa vijiweni wakipiga 'stori'. Pengine hawa ndio wanaamini kama alivyowahi kuimba msaanii mmoja kwamba eti "shibe ya nyumbani haina gharama!"

Taarifa zinazoumiza matumbo ni zile zinazoonesha kwamba, vijana wengi wa hapa mtaani kwetu, bila shaka na mitaa mingine, hawajiwezi kabisa katika kufanya kazi. Hata ukiwapa mtaji wajiajiri ni shiiida.

Kuna binti mmoja wa mtaani kwetu ninaambiwa alikabidhiwa duka kuuza ambapo mbali na mshahara waliokubalana na bosi wake, alikuwa na uhakika wa kupata kifungua kinywa na chakula cha mchana kwa pesa ya bosi.

Lakini kitendo cha kukaa dukani kuanzia saa mbili hadi usiku kimemshinda!

Kisa? Anakosa 'ubuyu', yaani kukaa kijiweni na wasichana wenzake 'wakipiga umbea'. Kwa lugha nyingine, kazi ya kuuza duka iliyokuwa inamwokoa na dhambi ya kusengenya, kuwazulia watu na kupelelezana ambayo baadhi ya dini zinasema ni katika madhambi makubwa, yeye akaona kwa kukaa dukani anakosa kitu muhimu!

Jamaa mwenye duka ambaye anaamini wasichana wengi angalau bado ni waaminifu kulinganisha na wavulala, kaleta binti mwingine kutoka mikoani na hivi tunavyoongea anendelea kupiga kazi!

Lakini kwa utafiti wangu nimegundua kwamba tatizo kubwa linalosababisha yote haya ni malezi mabaya ya watoto wetu.

Moja ya malezi hayo hatari ambayo makala hii inaangazia ni kuona watoto chini ya miaka saba, wakicheza au kumangamanga nje ya nyumba zao wakati mwingine hadi saa tatu usiku huku wazazi wakuwa 'wamerilaksi' tu.

Wale wanaotoka familia zinazokula mlo mmoja au miwili kwa siku hapo mtoto anaweza kumangamanga nje hadi saa nne usiku au zaidi!

Unashangaa kusikia watu wakila mlo mmoja kwa siku? Ni wengi tu mbona! Nakupa siri. Ukikuta eneo biashara ya miguu ya kuku, vichwa na utumbo imeshamiri kama mtaani kwetu, basi hapo hukosi kukuta idadi kubwa wakishindia mlo mmoja kwa siku au miwili!

Chakula kikuu ambacho hutengwa mezani kati ya saa 12 na saa moja jioni, mara nyingi huwa ni ugali wa sembe na mara mojamoja ubwabwa, kwa miguu ya kuku, maharage au dagaa mchele wa mafungu. Mchana hupita 'bilabila' na wale wanaobahatisha milo miwili hupata chai na mihogo ya kukaanga yaani 'chipsi-dume' kati ya saa tano na saa sita.

Pamoja na hali ngumu ya maisha, sehemu kubwa ya familia kuwa tegemezi huchangia hali hii ya umaskini.

Siku moja, baada ya kukuta watoto wakiwa mtaani saa tatu usiku huku wakishikana mashati kutaka kupigana na mimi kuingilia kati, niliamua kuwapigia hodi baadhi wazazi wao, hasa wale tunaofahamiana.

Nikauliza kama wanajua mahala watoto wao walipo muda huo, takribani wote walinipa jibu hili: "Mwanangu yuko hapo nje anacheza na wenzake."

Nilipouliza kama mzazi anajua mchezo anaocheza mwanawe na hao 'wenzake', baadhi ya majibu yalikuwa kama hivi. "Michezo yao ni hii ya kukimbiakimbia tu." "Hata sijui wanacheza nini lakini ni michezo tu ya kitoto". "Kwani wewe hujui michezo ya watoto?"

Hakuna aliyejibu sawasawa maswali haya niliyozidi kuuliza: Unawajua hao wenzake anaocheza nao ni akina nani? Wanatoka famia gani? Tabia zao zikoje?

Katika mafundisho ya dini na ya wataalamu wa malezi na saikolojia ambayo wazazi tunapaswa kuyafuata, ni pamoja na kuhakikisha watoto wanakuwa ndani ya nyumba baada ya saa 12 jioni. Huu ni muda unaosemekana pia kwamba mashetani huzagaa mitaani. Kumbuka mwanadamu pia huwa shetani kamili pale anapofanya mambo ya kishetani!

Kimsingi, kila mzazi ana dhima ya kujua marafiki wa mwanae ni akina nani na tabia zao na kujua hata tabia za wazazi wao. Kwa mfano, hupaswi kuruhusu mwanao kuwa rafiki wa mtoto ambaye mzazi wake anatuhumiwa kwa wizi, ushirikina, kutumia dawa za kulevya na tabia nyingine zisizofaa katika jamii.

Hili halipaswi kuishia mtaani tu, bali pia shuleni. Mzazi unapaswa kufuatilia kujua rafiki wa mtoto wako shuleni ni nani na hata uwezo wake wa darasani, tabia zake, kujua wazazi wake na kujua jinsi walimu wanavyomsema mwanao na rafiki yake aliyejichagulia.

Sasa hivi baada ya masomo, shule nyingi hutoa kazi za kwenda kufanyia nyumbani. Hivi mtoto anayecheza nje hadi saa tatu usiku anafanya kazi za shule saa ngapi? Mzazi unapitia saa ngapi kazi zake za shule na kumsaidia? Kwa waumini wa Kiislamu, kwa nini muda huu wa jioni mtoto asiwe msikitini ili kupata athari na mazoea ya kuswali sala za usiku au madrasa kwa kuwa siku hizi zipo madrasa za usiku?

Katika uchunguzi wangu nimegundua shida nyingine. Kwamba mtaani kwetu watoto wengi ambao muumini mwenzangu aliwaita wajukuu katika nyumba za urithi wamelelewa au wanalelewa na mama zao pekee (single parents). Hii imenikumbusha tafiti moja inayoonesha kwamba zaidi ya asilimia 70 ya wafungwa wa kesi za mauaji, ubakaji, ujambazi na wizi walilelewa na mama pekee.

Maana yake ni kwamba sauti ya baba katika malezi ya mtoto ni muhimu sana hivyo wazazi tujitahidi kuhakikisha mabinti zetu wanaolewa na si kuzalia nyumbani.

Wanaume pia tuepuke kuwapa mimba wanawake bila kuwaoa kwani tunachangia sana watoto hawa 'kula kulala' ambao baadhi yao hugeuka kuwa wahalifu.

'Single parents' pia mjue hili na muwe makini kwa kuchukua pia nafasi ya baba katika malezi.

Tujitahidi pia kuvumiliana kwenye ndoa kwani baadhi ya watoto hawa hujikuta wakilelewa na mama pekee baada ya ndoa kuvunjika. Kama nilivyojadili kwenye makala iliyopita, wanawake mjitahidi pia kuwaheshimu waume zenu, kuwapa furaha kwa kuepuka kuwakera ikiwemo kuwanyima unyumba. Kwani hayo mawili yanachangia sana wanaume kuchepuka na kuzaa hovyo au ndoa kuvunjika kabisa.

Watoto ni taifa la leo na kesho. Wana haki ya kupata malezi bora na sahihi ikiwemo kuhakikisha wanasoma vizuri, wanamjua Mungu na kufundishwa kupenda kufanya kazi.

Tukutane wiki ijayo.

Jamii



# Wanaowapa mimba wanafunzi stahiki yao ni jela

**Na Lauden Mwambona**

WAKATI akizindua ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiririia vya Malaria ya mwaka 2022 hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan aliutaja mkoa wa Songwe kwamba ndio unaoongoza kitaifa kwa kuwa na idadi kubwa ya mimba za utotoni.

Kutokana na utafiti huo, takwimu zilionesha kwamba kwa kila wasichana wadogo 100, karibu nusu yao, yaani wasichana 45 hupata mimba za utotoni kwa mwaka mkoani humo!

Mikoa inayofuata kwa uwingi wa mimba za utotoni ni Ruvuma wenye asilimia 37, Mkoa wa Katavi asilimia 34, Mara asilimia 31 na Mkoa wa Rukwa wenye asilimia 30.

Hali hiyo imefanya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alipotembelea mkoa huo hivi karibuni, moja ya eneo alilojikita ni hilo la kutafuta mwarobaini wa mimba za utotoni ambapo waathirika wakubwa ni wanafunzi.

Taarifa hizi mbaya zimekuja wakati Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan inapambana katika kuboresha miundombinu ya shule za msingi na sekondari nchini kote sambamba na kutoa elimu bila ada.

## WAHALIFU WASAKWE

Katika hatua za kuchukua ili kumaliza kama si kupunguza wimbi la mimba za utotoni, Waziri Mkuu amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk Francis Michael na wakuu wa wilaya zote za mkoa huo wahakikishe wanawasaka watu wote wanaotuhumiwa kuwapa mimba watoto wa kike na kuwafikisha kwenye mkono wa sheria.

"Tangu Januari hadi sasa, mkoa huu una matukio 59 za wasichana walioacha shule kwa sababu ya ujauzito lakini ni kesi mbili tu zimeenda mahakamani. Hizo 57 ziko wapi au zimeishia wapi? Ni nani anazuia kesi hizi zisiende? Jeshi la Polisi, ni kwa nini hatuwafikishi watuhumiwa kwenye vyombo vya sheria?" Anahoji Waziri Mkuu.

Anaongeza: "RC na Ma-DC wote kaeni na kamati zenu za ulinzi mbainishe wahusika na mhakikishe hatua kali zinachukuliwa dhidi ya wote waliohusika."

Anawaonya vijana wanaopenda kutembea na watoto wa shule waache tabia hiyo mara moja kwani wanafanya jambo ovu la kuwakatisha masomo na kuharibu maisha ya baadaye.

Anawakumbusha kuhusu kuozea jela wasiobadilika pale anaposema: "Sheria iko wazi katika kosa hili. Adhabu yake ni miaka 30... We kijana, kabla hujamfuata binti jiulize una miaka mingapi, sababu tukikufunga utarudi ukiwa mzee."

## WATOTO WA KIKE WALINDWE

Akisisitiza haja ya kuwalinda mabinti, Waziri Mkuu anasema: "Hawa ni watoto wetu, tunapaswa tuwalee ili wakue na kuja kushika majukumu ya nchi. Rais Samia amewekeza kwao kwa kutoa elimu bila ada. Tunapaswa tuhakikishe wanatimiza ndoto zao, kwa hiyo tuwalee ili waweze kuhitimu."

Anawaomba masheikh na wachungaji wakemee tabia hiyo kupitia mahubiri ya kwenye ibada na pia anawakumbusha wazazi jukumu la ulezi wakihakikisha hawasababishi watoto kujiingiza katika mambo yatakayosababisha kubebeshwa mimba.

## SONGWE WANAVYOJIPANGA

Kabla ya Waziri Mkuu kuja Songwe, Mkuu wa Mkoa huo, Dk Michael alieleza kusikitishwa sana na mkoa wake kuongoza kwa mimba za utotoni.

"Ni taarifa mbaya ambayo imenifanya kuitisha vikao mara moja ili kujua sababu, mkakati na kuchukua hatua ili kuzuia kadhia hii," anasema.

Dk Michael, anasema mkoa umeanza kuchukua hatua za kudhibiti mimba za utotoni ikiwa ni pamoja na kuunda timu ya wataalamu ili kuchambua chanzo na ukubwa wa tatizo.

Mkuu wa mkoa anasema katika vikao hivyo imegundulika kuwa kundi kubwa la watoto wanaopata mimba ni wale wanaomaliza darasa la saba, walioshindwa mitihani na wale wanaoacha shule kabla ya kumaliza darasa la saba.

Ofisa katika idara ya elimu anatoa mfano kwamba mwaka 2022, zaidi ya wanafunzi 29,000 wa darasa la saba walifanya mitihani, lakini waliochaguliwa ni wanafunzi 13,000 huku wengine 16,000 wakibaki mitaani.

"Upo uwezekano kwamba wasichana walioshindwa kuendelea walikuwa zaidi ya 8,000 jambo ambalo pia ni mwanya wa watoto hao kupata mimba," anasema Ofisa huyo bila kutaja jina lake.

# Jamii

**MITAZAMO POTOFU**

Akitoa maoni yake, Anastazia Mwashiuya (54), mkazi wa Kata ya Hasanga, Mbozi, anasema wakati mwingine mimba za utotoni zinachangiwa na mtazamo uliopitwa na wakati.

Anasema zamani ulikuwapo mtazamo hasi kwa msichana aliyemaliza darasa la saba kwamba hatakiwi akutwe na mdogo wake wa darasa la sita akiwa nyumbani bali anatakiwa awe ameolewa au yupo kwake. Anahisi pengine bado kuna wazazi wenye mtazamo huo.

Mkazi mwingine wa Kata ya Iyula, Mkaisa Mrisho (29) ana mawazo kama ya Anastazia kuhusu desturi kuchangia mimba za utotoni ambazo wanafunzi ndio waathirika wakubwa.

Yeye anasema ndoa za wakazi wa Mbozi zinahusisha pia mwanaume kumchukua kwa nguvu msichana anayempenda ili mradi awe na kuku mmoja ambaye anatumika kutoa taarifa kwa wazazi wa msichana huyo kwamba mtoto wao yupo kwa mwanaume husika.

Anasema akishatoa taarifa basi anapeleka jembe la mkono kwa wazazi wa msichana ili waunganishe ukoo na hapo ndoa imeimarika kwani mahari mengine yanatafutwa polepole.

**MWAMKO MDOGO**

Mrisho anasema watoto wengi wanaomaliza darasa la saba Songwe, hususani wasichana wanaolewa kwa njia hiyo lakini wengine wanaenda kufanya uyaya, wengine kwenye mabaa maeneo ya madini na jiji la Mbeya wakati wavulana wanakwenda kulisha mifugo na kwenye mashamba ya mpunga Mbarali mkoani Mbeya.


"Tatizo ni kwamba mwamko wa wazazi wengi mkoani Songwe kuwasomesha watoto shule hususani za binafsi bado ni mdogo, ndiyo maana asilimia kubwa ya wananoshindwa wanabaki nyumbani na kuishia kuolewa katika umri mdogo," anasema Mrisho.

Kuhusu wanafunzi wanaopata mimba Mkuu wa Mkoa anasema takwimu za wanafunzi kupata mimba zimepungua kulinganisha na miaka ya nyuma kwani kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Novemba ni wanafunzi wa kike 53 waliodhiruka kupata mimba .

Mkuu wa Mkoa anakiri kusikia habari za baadhi ya watu mkoani humo kumwona mtoto wa kike asiyepata mimba baada ya kumaliza darasa la saba kuwa na mkosi!

"Mila hii imetajwa kuwaaminisha hata wasichana wanaokosa wachumba kuamua kutafuta mimba kwa nguvu ili wadogo zao wanaomaliza darasa la saba wasiwawatangulie kupata watoto," anasema.

Anasema tatizo lingine ni wazazi wengi mkoani Songwe kumwona msichana ni kitega uchumi cha kupata ng'ombe za mahari hivyo watoto wengine wanalazimishwa kuolewa.



**ULEGELEGE VYOMBO VYA SHERIA**

Anataja sababu nyingine ya wanaume wa Songwe kuendelea kuwapa mimba wasichana mimba za utotoni kuwa ni utendaji wa mashaka wa vyombo vya kutoa haki hususan viongozi wa vijiji, kata, polisi, waendesha mashtaka na mahakama.

Anatoa mfano kama alioutoa Waziri Mkuu kwamba katika matukio ya wasichana zaidi 50 kupata mimba kuanzia Januari mwaka huu hadi Novemba ni kesi mbili tu zilizofunguliwa ikiwamo moja ya kijana aliyefungwa miaka 30, lakini nyingine kijana amefungwa kifungo cha nje mwaka mmoja, licha ya kutuhumiwa pia kwa ubakaji!

"Kutokana na hili nimepanga kuitisha kikao cha kamati ya Ulinzi na Usalama mkoa kitakachowashirikisha waendesha mashtaka, polisi wa upelelezi na mahakimu," anasema.

Mkuu wa mkoa anasema mkakati wa kwanza ni kuwasaka watuhumiwa wote wanaotuhumiwa kuwapa wanafunzi mimba na kuhakikisha wanafikishwa kwenye mkono wa sheria.

Mkakati mwingine anasema ni kuendelea na ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wasichana katika sekondari kutwa na kwamba shule za bweni kwa sasa zipo wilaya ya Ileje na Halmashauri ya Tunduma na hivyo ujenzi utafuata katija it aaaaaaahalmashauri za Mbozi, Momba na Songwe.

**VYUO VYA UFUNDI**

Lakini Diwani wa Kata ya Vwawa wilayani Mbozi, Mhe George Kiwaya anasema ipo haja kwa halmashauri kuhamasisha ujenzi wa vyuo vya ufundi ili watoto wengi wanaoishia darasa la daraja la saba wajiunge.

**AGIZO KWA NCHI NZIMA**

Agizo la Waziri Mkuu kuhakikisha wanaume wanaowapa mimba wanasakwa bila shaka halihusu mkoa wa Songwe pekee, bali Tanzania nzima, bara na visiwani.

Kwa hiyo tunatarajia kuona muda mfupi ujao wanaume wanaowapa mimba wanafunzi katika kila mkoa maarufu 'mafataki' wanafikishwa mbele ya sheria

**MADHARA MIMBA ZA UTOTONI**

Mimba za utotoni ni ukatili wa kijinsia kwani mara nyingi zinakatili mustakabali wa baadaye wasichana hawa wadogo, wakajikuta wanalea watoto wenzao badala ya kuendelea na masomo.

Inaelezwa pia kwamba kutokana na via vyao vya uzazi kuwa bado vichanga, watoto hawa wanapopata ujauzito hukumbwa na matatizo mbalimbali ya uzazi.

Wataalamu wa lishe wanasema kwamba mzazi anapaswa kujiandaa kabla ya kupata ujauzito kwa upande wa lishe ili asizae mtoto mwenye matatizo yatokanayo na lishe duni lakini mara nyingi hakuna maandalizi kwa watoto hawa wanapopewa ujauzito.

Baadhi ya matatizo yatokanayo na lishe duni ni watoto kuzaliwa na vichwa vikubwa au migongo wazi, kupata udumavu lakini pia wanaweza kupata uzazi pingamizi unaosababisha udumavu.

Udamavu ni tatizo hatari ambalo mtoto mwenye tatizo hilo ukuaji wake wa mwili na akili huwa duni kulinganisha na watoto wengine. Mtoto huugua mara kwa mara, darasani hawezi kufanya vizuri na hata kwenye ajira hafanyi vizuri. Waliopata udumavu wengi huzungukwa na umaskini wa kudumu.

Mbaya zaidi mtoto akishapata udumavu hata baadaye akila vizuri hawezi kufanana na ambaye hakupata udumavu maisha yake yote.

Udamavu hutokana na lishe duni kuanzia kwa mama tangu mimba inatungwa hadi mtoto anapofikisha umri wa miaka miwili (siku 1000).

**KWA NINI KUHANGAIKA NA WATOTO?**

Kimsingi, mwanaume anapohangaika na wanafunzi au wasichana wadogo hata kama hawako shule wakati mitaani kuna rundo la wanawake wanaotafuta wanaume ni mtu ambaye ni wa hovyo na hatari kwa ustawi wa jamii.

Kumekuwepo na tatizo la kuwashughulikia watu wanaowapa mimba wanafunzi kwenye vyombo vya sheria kutokana na wazazi kuchangia hali hiyo baada ya kuahidiwa rushwa na wahalifu na kuharibu ushahidi au kumaliza kesi nje ya mahakama.

Hali hii inachangia tatizo la uhalifu dhidi ya watoto kuendelea kushamiri na hivyo inapaswa kukomeshwa.

**SHERIA KALI KWA WAZAZI AINA HII**

Ni vyema vyombo vya sheria vikawachukulia pia hatua kali sana wazazi ambao wataonekana kutaka kuharibu ushahidi ili kuwalinda wahalifu hawa na pengine ni wakati mwafaka wa kuangalia pia sheria zetu na kuzirekebisha katika eneo ili ziwaguse pia wazazi wa aina hii.

Ni vyema pia watu wanaopatikana na hatia ya kuwapa mimba wanafunzi watangazwe sana kwenye vyombo vya habari, hatua itakayosaidia kuwatisha wahalifu wengine.

**ELIMU ZAIDI**

Lingine la muhimu ni wahusika, kwa maana ya viongozi, kuelimishwa kuhusu madhara ya mimba za utotoni ili nao waweze kuelimisha jamii kuhusu madhara ya mimba hizi.

Hii, sambamba na matumizi ya sheria, itasaidia sana kuzipunguza kama si kumaliza kabisa mimba za utotoni.

Mwisho



Uchumi

# Umasikini na maendeleo ya Tanzania - 3

**Na Dk. Felician Kilahama**



MKWAWA

NAMSHUKURU Mungu kwa namna anavyotujaalia amani pamoja na zawadi ya uhai na afya njema Watanzania wote.

Huu ni mwendelezo wa makala inayofafanua kuhusu kupima maendeleo/mafanikio ya Tanzania kwenye mizania moja na mataifa tajiri au yaliyoendelea kuwa pengine si jambo sahihi.

Sehemu ya kwanza ilimalizika kwa kuonesha kuwa wale wageni kutoka Ulaya waliokuja huku kwetu wakijulikana ni 'wavumbuzi' au 'wamisionari' walikuja Afrika kati ya Karne ya 14 na 18 wakitanguliwa na Waarabu kutoka Mashariki ya Kati waliofika Afrika tangu karne ya saba.

Pamoja na mambo mengine, wazungu kutoka Ulaya waligundua kuwa Afrika halikuwa bara lililo gizani bali limesheheni rasilimali, watu wenye nguvu na uwezo wa kufanya kazi pamoja na maliasili za kutosha.

Mataifa ya Ulaya yaliyokuja Afrika ni pamoja na Ujerumani, Ureno, Uingereza, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Hispania, na mengineyo. Kitu cha kwanza walichokifanya ni kugawana maeneo ya kutawala ili waweze kunufaika zaidi na raslimali zetu na wasigombane wao kwa wao.

Baada ya kugawana maeneo ya bara letu kati yao; mipaka ikawekwa na mataifa ya Afrika yakawa kwenye ramani kama walivyokubaliana hao wageni. Mipaka hii kwa sehemu kubwa ndio inayotumika hadi leo.

Wakoloni hao walifanikiwa kwa sababu walikuwa na nguvu za kivita, kimaarifa na kimiuondombinu kuwazidi mababu zetu hivyo, wakaweza kutekeleza azma yao barani Afrika kiulaini!

Hata hivyo, halikuwa jambo rahisi maana wakoloni walikumbana na upinzani mkali katika maeneo mbalimbali ikiwemo Tanzania kama vita vya Majimaji Songea, Mkoani Ruvuma na kule Kenya wakakumbana na vita vya Maumau.

Kwa hapa Tanzania, mbali na Majimaji, kulikuwepo mapambano sehemu nyingine nchini mathalani, kwa Chifu Mkwawa, Iringa kwa Chifu Milambo kule Tabora na sehemu nyinginezo.

Kama ilivyokwisha dokezwa, wakoloni walikuwa na nguvu kwa sababu mataifa ya Ulaya na Amerika wakati huo (karne ya 18), walishajijengea uwezo wa kutosha, kitaaluma na miundombinu ya usafiri na usafirishaji kama vile 'merikebu'. Isitoshe walikuwa na silaha za moto kama bunduki na risasi za kutosha.

Kwa upande mwingine, inafahamika kwamba Waarabu walianza kufanya biashara ya watumwa tangu karne ya saba na biashara hiyo iliendelea hadi miaka ya 1960 wakati baadhi ya nchi za kiafrika zilipoanza kupata uhuru.

Njia kuu mbili zilitumika katika biashara hiyo ya utumwa; kutoka Pwani ya Afrika hadi Mashariki ya Kati (Middle East). Pili, ni ile ya "trans-Saharan Caravan Traffic" ikiungana na biashara ya watumwa iliyoanzia Afrika Magaharibi kwenda Amerika Kaskazini na Kati (nchi za Caribbean) hadi Brazil (Amerika ya Kusini).

Vilevile, kupitia Pwani ya mashariki mwa Afrika, watumwa walipelekwa Uarabuni.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, biashara ya watumwa ilianzia Kaskazini hadi kusini mwa Afrika kwa kuunganisha maeneo ya Ethiopia na Eritrea pamoja na Somalia na kuteremkia Afrika Mashariki hadi eneo la 'Maziwa Makuu' mpaka Msumbiji.

Historia inaonyesha kuwa kutoka Afrika watu kati ya milioni 12 hadi 15 walipelekwa sehemu mbalimbali duniani.

Pamoja na hayo yote kufanyika Afrika, bado mataifa ya Ulaya yaliyotawala nchi mbalimbali; harakati hizo zilikuwa ni sehemu ya mikakati yao hasa ya kujiletea maendeleo yaliyochochewa na kukua kwa viwanda/uchumi takribani zaidi ya miaka 300 iliyopita.

Hali hiyo ilichangia sana kuwafanya waje Afrika baada ya kugundua kuwa zilikuwepo fursa za kutosha. Hivyo, Wakoloni walichukua rasilimali nyingi katika maeneo mbalimbali ya Afrika.

Pamoja na nguvukazi kubwa kuchukuliwa kama watumwa, pia walichukua madini mbalimbali pamoja na rasilimali nyingi kama madini, vito vya thamani, mbao, magogo na nguzo kutoka kwenye misitu ya asili.

Vilevile walipora mazao na malighafi za viwanda mathalani, pamba, kahawa, ngozi za wanyama kama chui, simba, mamba na kadhalika; meno ya tembo na faru pamoja na rasilimali nyinginezo walizoziona kuwa zina thamani kiuchumi na kijamii.

Kimsingi, wakoloni waliweza kuyafanya hayo kutokana na uwezo wa kimaendeleo na kiuchumi waliokuwa wameufikia. Wakati huo Afrika ilikuwa kwenye hali isiyoeleweka kielimu na kimaendeleo.

Maendeleo yaliyofanyika kwenye 'makoloni' husika, yalilenga kuwawezesha wakoloni kusafirisha malighafi, madini na bidhaa nyinginezo kutoka Afrika. Mathalani, hapa kwetu, Wajerumani na Waingereza walijenga reli ya kati hadi Mwanza na Kigoma; pia mpaka Arusha na Tanga na baadaye Kaliua mpaka Mpanda. Vilevile, ilikuwepo reli kutoka Tanga hadi eneo la 'Zigi' kwenye Msitu Asilia wa Amani Wilayani Muheza.

Kadhalika, zilijengwa bandari kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi na katika Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa) kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa bidhaa/malighafi na watumwa kwenda maeneo kusudiwa nje ya Afrika.

Je, hali kama hiyo iliashiria nini kwa mustakabali mzima kwa Afrika? Jitihada za mataifa ya Ulaya kuwa na makoloni katika Afriaka zilipelekea Bara letu kudhoofika kijamii, kiutamaduni na kimaendeleo.

Kupitia Kitabu kilichoandikwa na 'Walter Rodney (1972); mwandishi alieleza kinaganaga jinsi Afrika ilivyonyonywa kimakusudi na kutoendelezwa na wakoloni. Moja ya hoja zake kuu katika kitabu hicho, inasisitiza kuwa "Afrika iliendeleza mataifa ya Ulaya kwa kasi kubwa na wakati huohuo, mataifa ya Ulaya yaliifanya Afrika kuwa duni kwa takribani kasi hiyohiyo."

Tuseme nini juu ya hali hiyo? Ni hali ambayo haikutarajiwa maana kwa miaka mingi, Afrika ilidumaa kwa kupungukiwa nguvukazi yake muhimu pamoja na kuporwa kwa rasilimali zake muhimu hususani maliasili kama misitu, madini, wanyamapori na nyinginezo kutokana na dhamira ya wakoloni kuendeleza mataifa yao.

Tulipopata uhuru Desemba 9, 1961, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa nchi yetu, alitangaza mapambano ya kitaifa dhidi ya maadui watatu; maradhi, ujinga na imaskini.

Hivyo, ikawa ndiyo mwanzo wa juhudi za kujiletea maendeleo baada ya kutawaliwa/kudhoofishwa na wakoloni kwa miaka mingi. Vilevile, akatahadharisha kuwa Ulaya wameendelea sana wakati sisi tupo nyuma. Hivyo akasema tufanye kazi kwa bidii na maarifa kiasi kwamba Ulaya na Amerika wakiwa wanatembea sisi tukimbie tena bila kuchoka.

Taifa linatimiza miaka 62 tangu tujitawale na wakati huohuo bado tunapambana na maadui walewale kwa kiasi kikubwa.

Ndiyo, tumepiga hatua kiasi katika utoaji wa huduma za jamii na miundombinu katika sekta za afya (maradhi), elimu (ujinga) na uchumi (umaskini) lakini bado hatujfikia viwango takiwa ili kukidhi mahitaji kwa watanzania wote.

Bado mengi yanatakiwa kufanywa na kuendelezwa katika kukuza uchumi wa mtu mmojammoja, jamii na taifa zima kwa ujumla.

Kama taifa ni muhimu tuzidi kuiunga mkono serikali inavyopambana katika kuhakikisha kila mmoja wetu anapata riziki yake kila siku, iwe ni wakulima, wafugaji, wafanyakazi wa umma na sekta binafsi; wafanyabiashara na wajasiliamali.

Kwa kuwa viongozi wana mchango mkubwa katika kuharakisha au kurudisha nyuma maendeleo yetu, tunapoelekea kwenye chaguzi zijazo tuwe makini pia katika kuhakikisha tunapata viongozi watakaotanguliza maslahi ya nchi yetu mbele na si matumbo, uchoyo na ubinafsi wao.

Kwa maneno mengine, kila mmoja apambane ili kujitoa katika usemi wa "mradi mkono uende kinywani"; ukimaanisha kwamba mtu apate chakula mengineyo yatafuata. Nchi yetu bado ina raslimali nyingi zinazoweza kuharakisha maendeleo yetu ya kiuchumi.

Kwa hiyo ukiangalia, bado matatizo yetu ya leo yana kiini chake kwenye minyororo ya kikoloni kwani licha ya kutupatia uhuru wa bendera, wameendelea kutubana kwenye eneo la uhuru wa kiuchumi.

Hivyo, taifa linajikuta katika hali yenye changamoto kadhaa za kiuchumi, kitamaduni, kimaadili na kimaendeleo kwani mataifa yaliyoitawala Afrika, kama ilivyokwishakuelezwa, hawakuja kwa mtazamo wa kuendeleza Afrika; bali kujikwamua kiuchumi na kuendeleza mataifa yao.

Na kwa kuwa wakoloni Hawa walishaonja na kufahamu maendeleo maana yake nini; hawakuwa na ajizi isipokuwa kufanya kweli ili wajiendeleze zaidi kupitia nguvukazi kutoka Afrika pamoja na rasilimali nyinginezo nyingi kulingana na uwezo waliokuwa nao wa kuzichukua maana hapakuwepo na kizuizi cha maana.

Hata hivyo, maandiko matakatifu yanatutahadharisha kuwa "iwapo misingi ikiharibika, mwenyehaki atafanya nini?" Kabla ya wakoloni kuja Afrika, kulikuwepo misingi iliyowezesha wakazi wake kuyamudu maisha yao.

Kitendo cha kutawaliwa ikawa ndiyo chimbuko la kuharibika kwa misingi husika: kwa hali hiyo mwenye haki (mwananchi) atafanya nini? Ndiyo maana mwandishi wa kitabu cha 'How Europe Underdeveloped Africa' Walter Rodney (1972), akafafanua namna yalivyokuwa hadi kuisababishia Afrika kuzorota kiuchumi na kimaendeleo; kwa spidi ileile ya kuondoka kwa rasilimali Afrika na kuzipeleka Ulaya na kwingineko duniani.

*Itaendelea*

Afya

# Limao ni dawa, kiungo na sharubati



**Na Godfrey Sanga**

FIKIRIA tunda linaloweza kutumiwa kukuza uchumi, kutumiwa kama dawa, kiungo, sabuni, dawa ya kuua vidudu jemsi na pia kipodozi. Aidha unaweza kulila, kunywa maji yake, na kukamua mafuta yake. Tunda hilo lina rangi ya kupendeza, linapatikana ulimwenguni pote tena si ghali, huenda hata sasa una tunda hilo jikoni mwako. Hili si lingine bali ni limao!

Kwa kutojua, huko nyuma ungeweza kusikia mtu akisema: "Usile limao (au ndimu). Linakausha damu." Lakini ukweli ni kwamba limau halikaushi damu bali hondoa vitu vibaya mwilini kama mafuta yasiyohitajika na kadhalika. Ingawa limau ni tindikali (acid) lakini likiingia mwilini hubadilika na kuwa alkali (alkaline) kwa maana ya kuwa na kiwango cha kitu kinachoitwa kwa kitalaamu "pH" nyingi. Hii ni tofauti na baadhi ya vyakula ikiwemo nyama nyekundu ambavyo kabla hujavila huwa ni alkali lakini vikiingia mwili hugeuka na kuwa tindikali kutokana na kuwa na pH kidogo.

Hata hivyo, manufaa mengi yanayopatikana kwenye ndimu, pia hupatikana kwa 'ndugu yake' ndimu. Kwa upande wa tiba, limau limegundulika kutibu magonjwa mbalimbali kama vile vidonda vya kooni, matatizo katika mmeng'enyo wa chakula, matatizo ya meno, homa, kuvuja damu ndani ya mwili, baridi yabisi, kutibu malengelenge, kupunguza uzito kupita kiasi, matatizo katika mfumo wa upumuaji, kipindupindu na shinikizo la juu la damu. Pia ni dawa nzuri kwa ajili ya nywele na ngozi.

Kwa miaka mingi sasa limao linajulikana kama dawa kwa kusaidia kuongeza kinga ya mwili, kusafisha tumbo na hujulikana pia limekuwa likijulikana kwa kusaidia katika kusafisha damu.

### VITAMINI C

Kwa wanaokumbuka, wakati janga la Uviko 19 limeshika kasi, baadhi ya wataalamu wa afya walitaja tunda hilo kuwa na vitamini C ya kutosha katika kusaidia kupambana na ugonjwa huo hatari.

Kikemia, limao ni aina ya kemikali askobini ambayo binadamu haziwezi kuitengeneza kwa ajili ya mwili wake na hivyo anategemea kuipata kutoka kwenye vyakula vyenye weza kemikali hiyo likiwemo limao.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, vitamini C ni muhimu kwa ukuaji na ustawishaji wa mwili. Mbali na malimao, wanasema vitamini hiyo pia hupatikana katika vyakula vingi kama vile mboga za majani, nyanya, pilipili hoho, zabibu nyeusi, na stroberi.

Matunda ya jamii ya machungwa yakiwamo malimau ndiyo chanzo kikuu cha vitamini C. Kiasi cha vitamini C katika limau hutegemea mambo mengi, kama vile hali ya hewa ya eneo ambalo tunda hilo lilikuzwa, ubivu wa tunda, na hata mahali ambapo tunda hilo lilikuwa katika mti.

Mbali na vitamini C, limao pia lina vitamini B6, vitamini A, vitamini E, folate, niacin thiamin, riboflavin, pantothenic acid, shaba, kalsiamu, chuma, magnesium, potassium, zinki, phosphorus na protini.

Juisi ya limao ina faida kadhaa nyingi ikiwa ni pamoja na kuondoa mchanga katika figo, kupunguza kukakamaa kwa mishipa na hupunguza joto la mwili. Mfano wa kinywaji ambacho huondoa uchovu mwilini, juisi ya limao itakusaidia kubaki mtulivu na mpole au mtu mwenye kujisikia huru.

Limao husaidia pia kuzuia matatizo ya kisukari, kufunga choo, shinikizo la juu la damu, homa, husaidia mfumo wa mmeng'enyo wa chakula kufanya kazi vizuri na matatizo mengine mengi yakiwemo kuimarisha ngozi ya mwili, nywele na meno.

Utafiti uliofanywa na Chama cha Madaktari wa magonjwa ya mfumo wa mkojo cha Marekani (American Urological Association) unaonyesha kuwa juisi ya limao inaweza kuondoa au kuzuia kujitokeza kwa mawe kwenye figo au kama tayari yapo basi wanasema juisi ya limao iliyoongezwa mafuta ya zaituni huondoa mawe kwenye figo.

Unaweza pia kutengeneza juisi ya limao kwa kuchanganya na asali na kupata kitu wanachoita "lemonade".

Harufu ya limao pia imegundulika kwamba inasaidia hufukuza mbu, wakati huo huo kuinywa juisi ya limao iliyoongezwa mafuta ya zeituni husaidia kuondoa mchanga katika kibofu cha mkojo.

### UMENG'ENYAJI WA CHAKULA

Tafiti zinaonesha kwamba pale tumbo linaposhindwa kumeng'enya chakula, juisi ya limao husaidia kutibu tatizo hilo sambamba na tatizo la kufunga choo.

Limao hufanya kazi kama wakala msafisha damu na mwili kwa ujumla. Na hii inakuwa nzuri pale unapopata juisi yako ya limao baada ya chakula cha mchana au cha usiku.

### TIBA YA HOMA

Juisi ya limao inaweza kumtibu mtu anayesumbuliwa na homa, mafua au baridi. Limau husaidia kutibu homa kutokana na sifa yake ya kuongeza kiasi cha jasho mwilini.

### AFYA YA MENO

Juisi ya limao imetumika pia katika kulinda afya ya meno na watu kupata matokeo mazuri. Kama juisi ya limao itanyunyizwa juu ya jino linalouma inaweza kusaidia kuondoa maumivu pia. Unaweza kupata faida hizi kama utakuwa unapiga mswaki ukitumia dawa yenye limau ndani yake.

### KUTUNZA NYWELE

Juisi ya limao imejidhihirisha pia kuwa dawa nzuri kwa upande wa matatizo mbalimbali ya nywele. Juisi hiyo ikipakwa kwenye ngozi ya kichwa inaweza kutibu matatizo kama ya mba, kupotea au kukatika kwa nywele, na matatizo mengine yahusuyo nywele na ngozi ya kichwa.

Kama utakuwa ukisafisha nywele zako kwa kutumia juisi au maji ya limao moja kwa moja basi utazifanya nywele zako zipate mng'ao wake wa asili bila gharama yoyote ya ziada.

### KULINDA NGOZI

Kwakuwa juisi ya limao ni dawa ya asili dhidi ya bakteria, inaweza pia kutibu matatizo mbalimbali ya ngozi. Juisi ya limau inaweza kutumika kupunguza maumivu kwenye ngozi sababu ya kupigwa na jua, pia husaidia kupunguza maumivu kutokana na kung'atwa na nyuki. Juisi ya limao au majimaji yake yanaweza kutumika kupakaa juu ya ngozi na kutibu chunusi na ukurutu.

Limao pia hutumika kama dawa ya kukufanya usionekane mzee kwa kuwa yenyewe huondoa mikunjo na madoadoa ya ngozi.

Kunywa maji ya limao yaliyochanganywa na asali husaidia ngozi kuwa na afya bora zaidi na hata ukipekua huko sokoni utazipata baadhi ya sabuni ambazo zimetengenezwa kutokana na limau.

### MAJERAHA YA MOTO

Upakaji wa maji ya limao kwenye eneo la ngozi iliyoungua huweza kusaidia makovu kupotea na hii husaidia pia kwa mtu aliyepatwa na malengelenge au vipele vyenye maji maji yanayouma ndani. Na kwa sababu limao ni wakala wa kupooza au wakala mtulizaji, huweza kupunguza maumivu.;

### KUZUIA KUVUJA KWA DAMU

Limao lina sifa ya kudhibiti bakteria mwilini (antiseptic properties) na kugandisha damu. Sifa hizi mbili husaidia kusimamisha danu inayovuja kwa mtu aliyepata jeraha. Unaweza kutumia maji ya limau ukiweka kwenye kipande cha pamba na kuiweke puani kuzuia pua kuvuja damu.

### KUPUNGUZA UZITO

Ukinywa juisi ya limao iliyochanganywa na asali na maji ya uvuguuvugu, hasa asubuhi tu unapoamka nyumbani inaweza kusaidia kupunguza uzito. Yaani inashauri unywe hiyo juisi ya limao wakati hujatia chochote tumboni.

### MATATIZO MFUMO WA UPUMUAJI

Juisi ya limao husaidia pia katika kutuliza matatizo katika mfumo wa upumuaji hasa kwa watu wenye matatizo kama ya pumu. Kwa kuwa limau ina kiasi kingi cha vitamini C, husaidia kutibu na kutuliza matatizo ya muda mrefu kwenye mfumo wa upumuaji.

### KIPINDUPINDU

Magonjwa kama kipindupindu na malaria yanaweza kutibika au madhara yake kupungua kwa kiasi kikubwa kwa kutumia juisi ya limao. Hii ni kwa sababu ya uwezo wa malumao katika kusafisha damu

### BARIDI YABISI, MAUMIVU YA MIGUU

Limao au ndimu husaidia katika kusisimua uzalishwaji wa mkojo na kwa sababu hiyo inaweza kutibu baridi yabisi na maumivu ya kwenye mishipa. Husaidia kutoa nje bakteria wabaya na sumu mbalimbali mwilini. Limao hutumika pia kutuliza maumivu au miguu ya kuwaka moto.

### KUTIBU MALENGELENGE

Juisi ya limao inaweza kusaidia kukausha malengelenge au vipele ambavyo huwa na majimaji ambavyo hujitokeza mara nyingi chini ya unyayo au katikati ya vidole vya mikono.

### MAAMBUKIZI KOONI

Limao ni tunda ambalo pia limethibitika kusaida matatizo yanayohusiana na maambukizi kooni na hii ni kutokana na sifa yake kubwa ya kudhibiti bakteria mwilini.

### SHINIKIZO LA JUU LA DAMU

Unywaji wa juisi ya limao huwa pia na msaada mkubwa kwa watu wenye matatizo ya moyo kwa sababu limao huwa na kiasi cha kutosha cha potasiamu. Limau husaidia pia katika hudhibiti shinikizo la juu la damu, kizunguzungu, na uchovu sugu.

Makala

# Tunajiandaaje kuzuia ukeketaji mwaka huu?

Na Hamisi Kibari

JUMATATU wiki hii, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa mwaka 2023 katika Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa ya Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Katika hotuba yake, Waziri anawataka watu wasiishie tu 'kukomenti' kwenye mitandao ya kijamii kuhusiana na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa sababu suala la hilo ni la watu wote wanatakiwa kulizuia.

Katika uzinduzi huo uliyoandaliwa na Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (Wildaf), Waziri anasema baadhi ya watu wanalifanya suala la ukatili wa kijinsi kuwa linawahusu viongozi tu.

"Unakuta mtu tukio limetokea mtaani kwake na alikuwa anaweza kulizuia, lakini anasubiri lifike mtandaoni akomenti kwa kuuliza kwamba viongozi wako wapi. Tubadilike… Pia niwaombe Watanzania, zile mila na desturi zilizopita na wakati tuachane nazo. Tusiendelee kuzikumbatia," anasema Dk. Gwajima.

Moja ya mila potofu inayoendelezwa na ambayo inahusisha ukatili wa kijinsia ni ukeketaji ambayo imenipendeza kuimulika katika makala haya.

Hivi tunavyoongea shule za msingi na za sekondari zinaelekea kufungwa na zingine tayari zimeshafungwa kwa ajili ya likizo ya mwisho wa mwaka.

Hatua hiyo inakuwa ndio chanzo cha maandalizi ya shughuli zingine za kijamii kwa ajili ya watoto, hususani jando na unyago.

Kwa mikoa ya Pwani muda huu wa likizo baadhi ya watoto watachezwa ngoma, jambo ambalo pengine tunahitaji pia kulitazama kama jamii kutokana na madai kwamba zinachangia mimba za utotoni, lakini katika jamii nyingine watoto, hususani wa kike, watakumbana na unyama.

Ndiyo, ni unyama na ndio maana mwandishi mmoja, Joseph Sabinu aliwahi kuandika makala kwenye gazeti moja la kila wiki ikisema:

"Ukeketaji: Sherehe kwa jamii, mateso na ulemavu kwa mabinti."

Japo ni takribani miaka 10 imepita lakini ningali ninakumbuka nilipokwenda Tarime, mkoani Mara, Januari mwaka 2013.

Ilikuwa ni wiki chache baada ya baadhi ya wenyeji wa wilaya hiyo kushiriki katika matukio ya ukeketaji wa waziwazi, wakipandisha bendera na kufanya maandamano, mengine yakipita mbele ya vituo vya polisi licha ya ukweli kwamba ukeketaji ni kosa la jinai! Sina hakika kama hili linaendelea lakini liliwahi kutokea na kuwashangaza wengi.



Wakati ninahojiana na baadhi ya wananchi pale Nyamongo, wale wanaopinga mila ya ukeketaji walitupa lawama nyingi kwa sisi wanahabari, wanaharakati na serikali kwa ujumla kwamba mara nyingi tunaibuka baada ya tukio na kisha tunanyamaza kimya!

Lakini na mimi, kama anavyosema Gwajima, nikawa ninaona na wao hawatakiwi kusubiri waandishi wa habari na wanaharakati, bali kuripoti hasa wanapooona maandalizi.

Hata hivyo, pengine walikuwa na hoja kwani sina hakika kama makala nyingi za kupinga mila hii mbaya ya ukeketaji zimeendelea kuandikwa katika kipindi cha maandalizi kama hizi au kabla. Sina hakika pia kama wanaharakati wameendeleza juhudi katika wilaya korofi zinazoendeleza mila hii potofu.

Kwa upande wa serikali sina hakika pia kama mengi yamefanyika kuanzia elimu hadi matumizi ya sheria katika kuhakikisha kwamba ukeketaji unakoma hapa Tanzania. Lakini takwimu zilizotolewa hivi karibuni na Waziri Gwajima zilionesha kwamba ukeketaji umepungua na unaendelea kupungua lakini tunatakiwa kuumaliza kabisa.

Wakati niliambiwa kulikuwa na ngariba mmoja amefungwa pale Tarime wakati huo huku kesi moja ikiwa inaendelea pia, Mwandishi mmoja wa Serengeti aliniambia hajawahi kusikia kesi yoyote ya ukeketeji wilayani humo ingawa ukeketaji upo kila mwaka!

Lakini Yusuph Marare, mkazi wa Musoma mjini ambaye amekuwa akifanya shughuli za ulimaji wa barabara katika baadhi ya vijiji vya Tarime alinijibu: "Ukeketaji ni tukio kubwa sana. Huwa ni maandamano ya watu wengi wakiwemo ndugu na waalikwa hata kutoka nje ya Tarime. Ni sherehe inayoandamana na kula na kunywa na mifugo mingi kuchinjwa.

Watu wanajaa ndani ya kilometa hata mbili… Katika wingi huo huku kituo cha polisi kikiwa na askari wasiozidi 10 watawafanya nini hawa.

Na kwa kweli akiwepo askari wa kutaka kutibua jambo hilo, basi hatakaa salama, lazima ahame, vingenevyo ajiandae kugechwa (kukatwa mapanga)."

Nilipenda Sabinus alivyoandika namna ukeketaji unavyokuwa sherehe kubwa Tarime, watu wakachinja ng'ombe, wakala, wakanywa na kusaza lakini hao wanaowafanyia sherehe kubwa namna hiyo, yaani mabinti,wanakuwa wameachwa katika mateso na kubwa zaidi ni ulemavu wa maisha.

Mateso wanayoyapata mabinti hawa ni mengi kuanzia kwenye maumivu makali, kuuguza na wengine hufariki dunia na mbaya zaidi, binti anayefariki dunia katika tendo la ukeketaji maiti yake hutupwa mithili ya mnyama, kwa maana kwamba hazikwi kutokana na imani nyingine potofu kwamba maiti yake ni mkosi!

Yaani wakati tafiti za kidaktari zinaonyesha kwamba vifo kwenye ukeketaji vinatokana na mshituko (shock) kwa sababu ya kuvuja damu nyingi, ama msichana kupata maambukizi (infections) kutokana na tendo hilo kufanywa kwa kutumia vifaa duni tena bila ganzi, bado jamii imeendelea kuamini katika suala la mila, mizimu na uchawi kuwa ndio sababu ya vifo.

Lucy Lazack Mrimi (aliyekeketwa mwaka 1992) aliniambia hiyo miaka 10 iliyopita kwamba alikuwa anajifungua kwa matatizo na wauguzi wakamwambia kwamba ni sababu ya kukeketwa.

"Unajua niliwahi kuishi Kibaha (mkoani Pwani) ambako nilipata ujauzito wangu wa kwanza. Nilipata taabu sana wakati wa kujifungua na waguzi katika Hospitali ya Tumbi walinisimanga sana baada ya kugundua kwamba nimekeketwa... Nilipopata ujauzito wa pili (bado nikiwa mbali na Tarime), nilishikwa tena na kiwewe. Yaani wakati nahisi sijui kama nitajifungua salama nikawa ninawaza namna manesi watakavyonisema kutokana na kuketwa..."

Lucy alikiri pia kwamba kwa kuketwa imempunguzia sana hamu ya kufanya tendo la ndoa na mumewe. "Yaani sisi tuliokeketwa hadi ufike kilele inabidi mwanaume akuandae muda mrefu sana."

Kuhusu maumivu wakati wa kuketwa, Lucy aliniambia kwamba ingawa alikeketwa toka mwaka 1992, hadi wakati ninaongea naye akikumbuka maumivu aliyoyapata anawasikitikia sana watoto wa kike wanaoendelea kuzaliwa katika makabila yanayokeketa.

Na kuhusu maumivu wakati wa hedhi, Lucy alikiri kwamba wanawake wengi waliokeketwa hulalamikia maumivu makali wakati wa hedhi.

Lakini bwana mmoja pale Nyamongo, Bahati Matiku, aliniambia kwamba watu wengi hawajui madhara ya ukeketeaji zaidi ya maumivu wanayopata mabinti.

"Ingawa wapo wanaojifungua salama lakini wengi waliokeketwa wanajifungua kwa matatizo lakini wananchi hawaelezwi kinachotokea hospitalini ili wajue kwa undani tatizo la ukeketaji," alisema Matiku.

Binti mwingine aliyetaka jina lake lisitajwe gazetini mkazi wa Musoma Mjini, aliniambia: "Unaweza kumpenda mvulana, sasa taabu inakuwa pale mnapopanga kwenda kufanya mapenzi.

Unakuwa unahofia asigundue kwamba umemeketwa na unahakikisha hakushiki sehemu za siri. Hii ni kwa sababu unahisi akikushika zile sehemu atagundua uko tofauti kama alishawashika wale ambao hawajakeketwa. Kwa hiyo unafanya lile tendo ukiwa umeshaathirika kisaikolojia. Hauwezi kufurahia sana."

Ndio maana lazima jamii yetu ikomeshe ukeketaji; sherehe kwa jamii, mateso na ulemavu kwa mabinti. Kila mwenye jukumu\ alitekeleze kwa nafasi yake. Kama alivyosema Waziri Gwajima, msisubiri 'kukomenti' zuieni kwa kuripoti maandalizi kwa vyombo vya sheria.



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Mambo ambayo watu wenye nguvu ya akili hawayafanyi-4

TUMSHUKURU Mungu kwa kuendelea kutubariki kuiona siku nyingine. Si kwa mapenzi yetu bali mapenzi yake kwetu.

Kwa mara nyingine tena napenda kuwashukuru wale wote ambao wanafuatilia mada hii na kuwasiliana nami kutokana wanachonufaika nacho.

Makala iliyopita ilimalizika kwa kuangalia mambo mawili muhimu ambayo watu walio na busara na nguvu ya akili hawayafanyi kwenye maisha.

Mambo hayo ni kwamba hawatumii muda wao mwingi kujadili na kutafakari mambo yaliyopita, badala yake huwaza ya mbele. Lakini pia tukasema hawafanyi makosa yaleyale tena na tena.

Katika makala za nyuma zaidi, tuliorodhesha na kufafanua pia mambo ambayo watu walio na busara na nguvu ya akili hawayafanyi kwenye maisha. Kwamba mtu anapoamua kuyaacha mambo hayo ndiyo kunasababisha asonge mbele kwa haraka.

Lakini bahati mbaya sana ni kwamba, wenye nguvu ya kuyaacha haya miongoni mwetu ni wachache.

Wengi wanashindwa kuyaacha mambo haya na kujikuta wakiendelea kuishi maisha ya chini sikuzote.

Baadhi ya mambo mengine ambayo tumeshayatajani pamoja na kwamba wenye nguvu ya akilihawapotezi muda kwa kujionea huruma kwa kufikiriamajanga, mikosi na mitihani ya maisha inayowafikabali kusopnga mbele. Lingine tumeona ni nguvu zao kutowapa wengine kwa maana ya kutotunza hasira,chuki au kulipa visasi.

Pia tuliona kwamba watu wenye nguvu ya akili hupenda hufanya mabadiliko chanya kwa maana ya kuwa tayari kubadilika wakishaamini kwamba jambo fulani lina faida kwao kama vile kufanya mazoezi au kudumu na ibada. Hawaishii kutamani tu moyoni kwamba nitafanya kesho, nitafanya kesho na kesho kuzaa kesho bali hufanya kweli mara moja.

Pia tuliona kwamba watu wenye nguvu ya akili hawahangaishwi na vitu wasivyoweza kuvidhibiti, hawahangaiki kwa ajili ya kuwapendeza watu wote na pia hawaogopi kuamua na kuchukua hatua.

Leo tunaendelea na mambo mengine ambayo watu wenye nguvu ya akili hawapotezi muda kuyafanya.



### HAWANA CHUKI KWA MAFANIKIO YA WENGINE

Kuwa na chuki ni kama kunywa sumu na kisha kudhani kwa sumu hiyo itsmuua adui yako.

Wivu unaweza kuelezewa kama; 'Ninataka ulicho nacho' wakati chuki kwa mafanikio ya mtu mwingine huenda mbali zaidi: "Ninataka ulicho nacho na sitaki wewe uendelee kuwa nacho". Yaani ni kuombea neema ambazo mtu kapewa na Mwenyezi Mungu zimtoke hata kama wewe hunufaiki lolote hata kama neema hizo zitamtoka.

Wivu ni wa kawaida kwa mwanadamu lakini inatakiwa wa kimaendeleo, yaani wa kuiga au kufikiria ufanye nini ili kumfikia yule unayemhusudu.

Lakini chuki ni mbaya kiafya na mustakabali wako. Chuki inayotokana na kukerwa na mafanikio ya wengine ni matokeo ya kutojitambua, kutojiamini na kutokuwa na furaha binafsi.

Chuki inaweza kukusababishia matatizo kama vile kutoweka mkazo katika njia yako ya mafanikio, kutoridhika na ulicho nacho na kuacha misingi yako na kupuuza ujuzi na vipaji vyako.

Inaweza pia kukufanya kuanzisha tabia ya kujisifu mwenyewe, kuharibu mahusiano yako na wengine, kujiona huna thamani au bahati na kadhalika.

Baadhi ya vitabu vya dini vinafundisha kwamba ukiona mtu amepata mafanikio, mwombee dua azidi kufanikiwa na kwamba mafanikio hayo yawanufaishe wengi pia jiombee dua Mwenyezi Mungu akupe neema na mafanikio kama hayo au zaidi.

Katika kudhibiti chuki zako na madhara yake, anza kwa kubadilisha mfumo wa maisha yako.

Badilisha kabisa mtazamo na saikolojia yako na anza kujiona mtu wa maana na fanya vile wanavyofanya watu wa maana.

Epuka kujilinganisha na wengine. Achana na dhana (hisia) kuhusu watu bali pata ufahamu na uhalisia kuhusu watu sababu unaweza kudhani wanafanikiwa sababu wana akili sana, kumbe wanatumia nguvu za giza au wanaiba au ni wabadhilifu nk.

Pia acha kutazama udhaifu wako tu, acha kuzikuza nguvu za wengine angalia zako. Usichukie wala kuyasemea vibaya mafanikio ya watu wengine. Acha kuwa mhukumu, fanya linalokupasa na zingatia ushirikiano badala ya ushindani.

Huwezi kuwa na mahusiano na watu unapofikiria tu jinsi ya kuwashinda badala ya kuwajenga.

Kuwatazama watu kama washindani sio jambo lenye afya kwa mahusiano yako badala yake, anza kuwaona kama sehemu ya timu yako.

Hii itakusaidia kuwa na watu wenye ujuzi na vipaji mbalimbali jambo ambalo linaweza kuwa na manufaa kwako. Epuka chuki sababu watu wenye nguvu ya akili hawana chuki kwa mafanikio ya watu wengine.

### HAWAKATI TAMAA BAADA YA KUSHINDWA

Kushindwa ni sehemu ya mchakato wa mafanikio. Kukwepa kushindwa ni kukwepa mafanikio. Wengi tunahis kwamba ikiwa tulishindwa mara moja, tutandelea kushindwa tena, hivyo hatuoni sababu y kufanya tena.

Hofu ndio sababu kuu y kutokutaka kujaribu tena kitu baada ya kushindwa. Badal ya kukabiliana na hofu, weng wanajiepusha na hatari y kushindwa tena ambay tunaihusisha na aibu.

Kuacha kunaweza pia kuw tabia mtu aliyojifunza tangu utoto. Lakini pia watu weng huacha sababu wana mtazam flani wa kudumu kuhusu uwez wao.

Hawana hakika juu ya kiwang chao cha kipaji, hivyo hawajal kuboresha na kujaribu ten baada ya kushindwa.

Wanaamini kwamba kam hawakuzaliwa na kipaji ch kufanya kitu fulani, hakun sababu ya kujaribu kujifunza Hivyo hofu yako ya kushindw inazuia uwezo wako w kujifunza. Mtazamo usi sahihi ukidumu, unaathiri jins unavyofikiri, kuhisi na kutend kuhusu kushindwa.

Mfano wa mambo ya kuepuk ni kama yafuatayo: mtazam kuwa kushindwa hakukubaliki kushindwa ni makosa yangu nilishindwa kwa sababu mim ni mbaya, watu hawatanipend ikiwa nitashindwa, ikiw sikufanikiwa kwanza, sitawez kufanikiwa mara ya pili, Mimi s mzuri vya kutosha kufanikiwa nk.

Badilisha mawazo hay yasiyo na msingi na siku zot kumbuka mtazamo sahihi kam vile; kushindwa ni sehemu y safari ya mafanikio, ninajifunz kutokana na kushindwa, nin nguvu ya kushinda hata baad ya kushindwa iwapo nitachagu kuendelea mbele.

Mtazamo huu utakusaidi na kukupa mtazamo w kukabiliana na changamoto n kusonga mbele hata baada y kushindwa.

Epuka kukata tamaa sababu watu wenye nguvu ya akil hawakati tamaa, wanajifunza n kusonga mbele.

Wework Consult - Your Partne in Growth.

**Itaendelea wiki ijayo...**



Na Hamisi Kibari

Mtanzania wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 10

**Mkewe anaporejea ghafla, kunatokea mtafaruku baada ya kukuta Chris ameleta nyumbani hawara. Chris anampiga mkewe ili kumteta hawara hadi kupoteza fahamu na kulazimika kumpeleka hospitali baadaye. Hata hivyo, anawadanganya ndugu wa mkewe kwamba mwanamke ametoweka akimwacha mwanawe mdogo na kwenda kusikojulikana. Daktari anayemtibu mkewe katika wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu anamjulisha kwamba mkewe amefariki dunia. Daktari huyo anampa njia itakayosaidia asishitakiwe kwa mauaji kutokana na kipigo alichomshushia. Chris anakubali njia hiyo lakini gharama za kuficha kifo hicho ni kubwa. Je, atazimudu? Ndugu wameanza kumtafuta mkewe na tayari wamefika polisi. Nini kitaendelea? Fuatana na mtunzi katika kisa hiki.**

Baada ya kutoka kwenye kaunta ya kituo cha Polisi, Jacob alimgeukia Mama Kessy: “Mimi ninashauri sasa twende hospitali tukamtazame mawodini na mochwari.””Lakini polisi wamesema kama wifi angekuwa na tatizo lolote wangekuwa na taarifa… Pengine si vibaya tukienda sasa hivi lakini ninashauri twende kesho. Unaonaje?””Mwalimu, ingefaa twende leo. Nitachukua teksi ituzungushe,” alijibu Jakob.”Ninaomba unisamehe, ninatakiwa ofisini. Nilikudokeza kwamba mimi ndiye mwalimu wa zamu wiki hii. Inabidi niwahi.””Haya, basi jioni tutakupitia na Mzee twende tukamsikilize huyu bwana (Chris), lakini kitendo cha dada kutofahamika alipo kinanitia wasiwasi sana,” alisema Jacob akiagana na Mwalimu Misango aliendelea kumtia moyo na kumtakaza asimwombee mabaya mdogo wake.* * *Mwalimu Misango alikuwa jikoni akiandaa chakula cha jioni akiwa na msichana wake wa kazi wakati mlango wa sebuleni ulipogongwa. Aliangalia saa kwenye simu yake. Ilikuwa inaelekea saa moja juu ya alama jioni. Akaenda kufungua.

Kama alivyotazamia, wageni walikuwa wameanza kuingia kwani kikao siku hiyo kuhusu mustakabali wa ndoa ya Mama Kenny ambaye bado alikuwa hajulikani alipo na mumewe, kilikuwa kinafanyikia nyumbani kwake.

Hii ilikuwa ni baada ya jana yake kikao kuahirishwa kwa maombi ya Chris aliyedai kuna taarifa muhimu kuhusu mkewe alikuwa akizitazama usiku huo na hivyo kuomba kikao kiahirishwe hadi siku iliyokuwa inafuata usiku.

Mwalimu Misango alipanga kikao kianze saa moja na nusu huku akiamini kwamba kingechukua wastani wa nusu saa kwa sababu hakuona kama kulikuwa na mambo mengi ya kuongea.

Ni kutokana na hilo, alikuwa anaandaa pia chakula cha usiku kwa ajili ya wageni wake.

Wageni waliokuwa mlangoni hawakuwa wengine bali Jacob ambaye jioni hiyo aliamua pia kuja na mkewe pamoja na baba yake mdogo, Mzee Chitawo Manyinyiri, yaani baba wa Tausi, maarufu Mama Kenny.

Mbali na mumewe aliyekuwa akimtazamia kuingia muda wowote akitokea kwenye shughuli zake, mtu mwingine muhimu katika kikao cha siku hiyo aliyekuwa akimtarajia kufika muda wowote ni mdogo wake, Chris.

Kwa mara ya mwisho alipowasiliana na mdogo wake huyo kwa simu alimhakikishia kwamba angekuja kwenye kikao hicho ambacho sasa kilikuwa kinafanyikia nyumbani kwake na kutoa taarifa mahala alipofikia katika juhudi za kumsaka mkewe aliyetoweka.

Wakati mwanzo malengo yalikuwa ni kusuluhisha na kutafuta mwafaka wa ndoa ya Chris na mkewe, sasa kikao kilijielekeza zaidi katika kujua aliko Mama Kenny na hatua za kuchukua kutokana na majibu ambayo Chris angeyatoa jioni hiyo.

Saa moja nusu Mwalimu Misango alijiunga na wageni wake baada ya kuhakikisha chakula kilikuwa tayari na kumwachia msaidizi wake wa kazi mambo madogo yaliyokuwa yamebaki pamoja na kuanza kuaandaa vyombo vya kupakulia chakula. Wakati huo mumewe alikuwa ameshawasili na kuungana na wageni sebuleni ambao walikuwa wakiburudika kwa juisi ya mchanganyiko wa embe, parachichi na passion. Ilikuwa pia imetiwa tangawizi kwa mbali.

Hata hivyo, Chris alikuwa hajawasili hadi muda huo. Baada ya kuketi huku akiangalia saa kwenye simu yake, Mwalimu Misango alipiga simu ya Chris lakini iliita bila kupokelewa.

Alijaribu kuipiga tena lakini kama mwanzo haikupokelewa.

“Vipi, unampigia mdogo wako, siyo?” Alihoji mumewe, Mhandisi Jacton Misango naye ‘akimwagilia moyo’ kwa juisi tamu.

“Ndiyo. Lakini hapokei simu.”

“Bila shaka atakuwa anakaribia kufika hapa nyumbani na ndio maana hapokei simu. Si alikuthibitishia atakuwepo kwenye kikao?”

“Ndiyo… Haya ngoja tumsubiri.”

**Tulipoachana jana, na hasa baada ya kikao kilichotakiwa kifanyike kuahirishwa, niliamua kwenda hospitali peke yangu kujaribu kumtafuta dada. Kwamba tusije tukawa tunadhani huyu mtu ni mzima kumbe yuko mochwari.**

Jacob ambaye alionekana ana mawazo mengi alifungua kinywa chake baada ya kimya kifupi kupita. “Wakati tunaendelea kumsubiri shemeji, kuna jambo nilitaka kuwajulisha.””Tuambie,” alisema Mwalimu Misango.”Tulipoachana jana, na hasa baada ya kikao kilichotakiwa kifanyike kuahirishwa, niliamua kwenda hospitali peke yangu kujaribu kumtafuta dada. Kwamba tusije tukawa tunadhani huyu mtu ni mzima kumbe yuko mochwari.””Enhe! Umegundua nini huko hospitali,” akahoji Mwalimu Misango.”Nilikwenda hospitali ya Kitete lakini jina la dada, nimefika hadi mochwari, halipo. Nimetembelea pia hospitali nyingine kubwa hapa Tabora lakini sikupata habari yoyote kuhusiana na Mama Kenny. Hata hivyo, kinachonishangaza, tangu juzi shemeji hataki kupokea simu zangu.”

“Pengine ni kama alivyoeleza dada yake hapa. Jana alikuwa bado hana majibu ya kueleweka. Ngoja tumsikie leo,” aliingilia kati Mhandisi Misango.

“Lakini hata leo nimempigia simu mara mbili hajapokea.”

“Pengine alijua kila kitu atakisema kwenye hiki kikao. Ngoja tuvute subira,” alisema Mhandisi Misango ambaye bado alikuwa ana mahusiano mazuri na shemeji yake, Chris na akimwamini. Hata yaliyokuwa yanatokea alijua ni mapito tu kwa sababu hata yeye kuna wakati alikuwa na ugomvi mkubwa na mkewe baada ya mkewe kugundua kwamba alikuwa na uhusiano fulani na msichana mmoja jirani yao. Hiyo ilitokea baada ya kunasa jumbe za maandishi kwenye simu ya mumewe na kuamua kufuatilia.

Waliendelea kumsubiri Chris hadi ikagonga saa mbili usiku bila kutokea. Mwalimu Misango alimpigia tena simu lakini kila wakati simu yake ikawa inaonekana kama inaongea na baadaye ikawa haipatikani kabisa.

“Alinihakikishia huku akiapa mara mbilimbili kwamba lazima atakuja. Sijui ni nini kimempata,” alisema Mwalimu Misango.

Ilipofika saa mbili na robo usiku, Mwalimu Misango aliamua kuwapa wageni wake chakula cha usiku.

Wakati wakiendelea kula, Mwalimu Misango alisema kama Chris hatotokea kabisa atalazimika kumwibukia nyumbani kwake alfajiri na mapema.

Jacob aliunga mkono akisema hata yeye atakuwepo. Mzee Chitawo naye akasema atakuwepo pia lakini Jacob akasema si vyema kumsumbua asubuhiasubuhi kwa jukumu ambalo alisema anaweza kulitekeleza bila tatizo.

“Mzee wewe utabaki tu nyumbani. Yatakayojiri nitakufahamisha,” alisema Jacob.

“Kwani Mama Kessy unatarajia kwenda kwa shemeji alfajiri ya saa ngapi?” Alihoji mumewe, Mhandisi Misango.

“Saa 12 juu ya alama nataka niwe pale.”

“Hakuna sababu ya kuwahi kiasi hicho. Ninajua shemeji yangu ni mtu wa kuamka saa mbili. Kwa hiyo hata mkienda saa moja inatosha. Watu wengi hatupendi kuamshwa asubuhiasubuhi kama jambo lenyewe linaweza kudubiri hadi saa mbili. Basi angalau ingekuwa saa moja,” alizidi kushawishi Mhandisi.

“Hapana” alikataa Mwalimu Misango. Akaendelea. “Tena nilitamani hata saa 11 niwe nimeshawasili kwake. Mtu wa aina hii ambaye anaahidi kitu muhimu kama hiki halafu hatekelezi ni kumwahi alfajiri. Sema tu siku hizi ni mtu wa kukesha baa tungemfuata usiku huuhuu lakini tukienda sasa hivi hatuwezi kujua atarejea saa ngapi.”

Jacob alimuunga mkono Mwalimu Misango akiahidi kuhakikisha anakuwa kwa Chris kabla ya saa 12 asubuhi.

“Shemeji anatufanya kama watoto wadogo. Mimi siamini kama ana dharura yoyote. Na ndio maana alikuwa hapokei simu zangu na sasa kaamua kabisa kutuzimia simu. Huwezi kuamini kwamba yule mtu muungwana ambaye mimi nilikuwa ninajivunia kwamba nina shemeji wa nguvu, ndiye kabadilika hivi.”

Baba yake mdogo anamgeukia: “Jacob, acha kumdhania mtu dhana mbaya. Tuchukulie kwamba amepata dharura… Mimi nadhani Mwalimu mjaribu tu kumwona kesho msikie anasemaje.”

* * *Jacob aliwasili kwa Chris saa kumi na mbili kasoro dakika kumi. Kwa jinsi mlango ulivyokuwa umefungwa alihisi hata Mwalimu Misango hajafika.

Alitaka kugonga lakini akasita, akaamua kusimama pembeni akisubiri. Baada ya dakika sita hivi kupita alimwona Mwalimu Misango akiwasili kwa pikipiki.

“Hapa ni kwa shemeji yako. Kwa nini unabaki nje?” Alihoji Mwalimu Misango akijongea kwenye mlango mkubwa wa nyumba ya Chris baada ya kumwona Jacob akiwa kasimama nje ya nyumba. Ofisa huyo wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora hakujibu kitu zaidi ya kutabasamu na kumsalimia.

Mwalimu Misango alibisha hodi mlangoni kwa Chris. Baada ya kubisha mara tatu, mlango ukafunguliwa na Chris ambaye alikuwa amevaa kaptula ndefu ya kulalia na fulaa. Akabaki kwa sekunde kadhaa akitazamba uso kwa uso na dada yake. Chris akakunja uso.

Mtu mwingine akaja nyuma ya Chris kuchungulia akiwa amevaa gauni la kulalia. Alikuwa Joyce. Mwalimu Misango akakunja uso macho yao yalipokutana.

*Itaendelea.*



# Vijana sita waburuzwa kortini tuhuma za mauaji ya malimu

**PARIS, Ufaransa**

VIJANA sita wamefikishwa mahakamani mjini Paris kwa tuhuma za kuhusika katika mauaji ya Mwalimu Samuel Paty.

Vijana hao wanatuhumiwa kwa kashfa na kumwelekeza Mwalimu Paty kwa muuaji wake, mkimbizi wa Chechnya, katika shule hiyo.

Walikuwa na umri wa kati ya miaka 13 na 15 wakati wa mauaji hayo mwaka wa 2020, huku kesi hiyo ikiendeshwa bila ya watu.

Vyombo vya habari vya eneo hilo, vinaripoti kuwa washukiwa hao, ambao wanakabiliwa na kifungo cha hadi miaka 2.5, walificha utambulisho wao walipofika katika Mahakama ya Watoto juzi Jumatatu.

Mwalimu Paty alidungwa kisu na kukatwa kichwa Oktoba 16, mwaka 2020 baada ya kuripotiwa kuwaonyesha wanafunzi katuni za Mtume Muhammad wakati wa darasa la uhuru wa kujieleza.

Mshukiwa mdogo zaidi alikuwa na umri wa miaka 13 wakati wa mauaji hayo. Alisimamishwa shule siku tisa kabla ya mauaji ya Malimu Paty kwa sababu zisizohusiana na kesi hiyo.

Alifika mahakamani huku kichwa chake kikiwa kimefichwa kabisa kwenye kofia ya koti jeusi chini, kwa mujibu wa Shirika la Habari la AFP.

Anadaiwa kumwambia baba yake bila ukweli kwamba aliadhibiwa kwa kumkabili Mwalimu Paty kwa madai ya kuwataka wanafunzi Waislamu kuondoka darasani.

BBC.



# Watu 11 wafariki dunia mgodini Afrika Kusini

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**

WATU 11 wamepoteza maisha katika mgodi wa madini ya platinam nchini Afrika Kusini, kwa mujibu wa Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Implats.

Ajali hiyo ilitokea juzi mchana katika eneo la Impala Rustenburg Jimbo la Kaskazini Magharibi.

Msemaji wa kampuni aliiambia idhaa ya kidijitali ya Afrika Kusini eNCA kwamba, watu 88 walihusika katika tukio hilo na kwamba watu 11 walipoteza maisa kutokana na majeraha.

Aidha, Msemaji wa kampuni hiyo aliongeza kuwa operesheni ya uokoaji ndani ya mgodi imekamilika.

Taarifa ya kampuni ilisema tukio hilo lilihusisha kamba iliyounganishwa na usafirishaji wa wafanyikazi, ambayo huwapandisha watu juu na ndani ya mgodi.

Usafirishaji unajumuisha ngazi tatu, kila moja ikiwa na uwezo wa kubeba watu 35, Implats ilisema.

BBC.

# Niger yabatilisha sheria kukomesha wahamiaji



**NIAMEY, Niger**

UTAWALA wa kijeshi Niger, umebatilisha sheria ya kudhibiti uhamiaji nchini humo ambayo iliharamisha kusafirishwa kwa wahamiaji kupitia nchi hiyo.

Utawala huo ilitangaza kufuta sheria hiyo katika taarifa yake ukibainisha kuwa Kiongozi wa Kijeshi, Jenerali Abdourahamane Tchiani, alitia saini amri ya kuibatilisha.

Sheria hiyo iliyopitishwa mwaka 2015 ikiungwa mkono na Umoja wa Ulaya ili kudhibiti wimbi la wahamiaji kutoka nchi za magharibi mwa Afrika wanaoelekea Ulaya.

Ilipingwa na wakazi wa jangwa ambao uchumi wao ulitegemea wahamiaji.

Kuna hofu kuwa kubatilishwa kwa sheria hiyo, kutarejesha wimbi la wahamiaji wanaopitia Niger kuelea Libya au Algeria kwa lengo la kufika Ulaya.


Wachambuzi wanasema hatua hiyo inaashiria kuwa serikali ya kijeshi inadai mamlaka yake kinyume cha shinikizo la kimataifa.

Inasemekana kwamba Niger ilipokea takriban Dola bilioni 1.9 katika usaidizi unaohusiana na uhamiaji kati ya mwaka 2015 na 2022.

Bado haijabainika wazi jinsi EU itajibu kile ambacho sasa kinaonekana kuwa pigo kubwa kwa mkakati wake wa kudhibiti mmiminiko wa wahamiaji kutoka Afrika.

BBC.

# Israel yawaachia huru wafungwa 33 zaidi wa Kipalestina



**YERUSALEM, Israel**

WAFUNGWA zaidi wa Kipalestina sasa wameachiliwa kutoka magereza ya Israel, kwa mujibu wa na mashirika mbalimbali ya habari.

Ikinukuu vyombo vya habari vinavyohusiana na Hamas, Reuters inasema walioachiliwa ni watoto 30 na wanawake watatu.

Shirika la habari la AFP, likinukuu mamlaka ya magereza ya Israel, linasema wafungwa 33 wameachiliwa. Haielezi ni wangapi ni watoto na wanawake.

Awali, Hamas na Qatar, zote zilisema Wapalestina 33 walipaswa kuachiliwa watoto 30 na wanawake watatu.

Inakuja kama sehemu ya mapatano yaliyokubaliwa na Israel na Hamas, ambayo ni pamoja na kusitisha mapigano na yameongezwa kwa siku mbili zaidi

Kwa usiku wa nne mfululizo, kundi la mateka wa Israel limebadilishwa na kundi la wafungwa wa Kipalestina chini ya mapatano ya muda kati ya Hamas na Israel.

Siku ya Jumatatu, wapatanishi wa Qatar walitangaza kuongeza muda wa siku mbili wa kusitisha mapigano, ikijumuisha Jumanne na Jumatano.Ikulu ya Marekani ilithibitisha kurefusha muda huo, lakini Israel bado haijafanya hivyo.

Umoja wa Mataifa, umetumia utulivu katika mapigano kuongeza usambazaji wa misaada ya haraka kwa raia wa Gaza lakini imeonya shehena hizo ni chache .

Wananchi wa Gaza wamekuwa wakitumia muda huo ili kupata vifaa na kuzuru eneo zima mara nyingi kurejea makwao na kutathmini uharibifu na kutafuta nguo za majira ya baridi huku hali ya hewa ikibadilika baada ya mvua na upepo kuanza.

# Mahakama yaamua 1.5% ya tozo ya nyumba kinyume cha Katiba



**NAIROBI, Kenya**

MAHAKAMA nchini Kenya, imeamua kuwa asilimia 1.5 ya ushuru ya nyumba iliyowekwa na serikali kama sehemu ya sheria ya fedha Julai, mwaka huu, ni kinyume cha Katiba.

Jopo la majaji watatu liliamua kwamba ushuru huo haukuwa na mfumo kamili wa kisheria na haukuwa na mantiki

Kuanzishwa kwa ushuru wa nyumba, miongoni mwa kodi nyingine, kulichochea maandamano watu wakilalamikia gharama kubwa ya maisha.

Serikali imeiomba mahakama kusitisha hukumu hiyo kwa siku 45 kupata muda wa kuamua hatua inayofuata.

BBC.

# Wanasoka nyota wadogo watakaobadili historia

**Na Valensi Mbaga**

WAKATI Lionel Messi na Cristiano Ronaldo wakiamua kuondoka Ulaya kwa ajili ya kutafuta maisha yao mazuri, mashabiki wa soka wana hamu ya kugundua ni wachezaji gani watachukua kijiti kama wachezaji bora zaidi duniani. Wapo vijana wadogo ambao wanatazamiwa zaidi kuja kufanya mambo makubwa na wafuatao ni wale waliofanya vizuri zaidi katika kona mbalimbali za soka duniani.




**10. Alejandro Garnacho (Man Utd)**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Argentina chini ya umri wa miaka 20 mwenye umri wa miaka 18 ameonyesha kiwango kizuri na kuonekana kuja kuleta kitu kikubwa baadae katika soka.

Garnacho amecheza na Cristiano Ronaldo katika ngazi ya klabu na amekuwa pamoja na Lionel Messi katika ngazi ya kimataifa hivyo amekuwa na mwongozo bora kwenye mchezo huo.

Garnacho ni winga anayesisimua na mjanja, ambaye tayari ameshafunga kwenye Ligi ya EPL kwa United. Anapata muda wa kawaida wa mchezo chini ya Erik ten Hag na ataimarika zaidi kama atapata muda zaidi wa kucheza.

**9. Youssoufa Moukoko (Borussia Dortmund)**

Anayefuata ni Youssoufa Moukoko anaekipiga Borussia Dortmund. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 18 aliingia uwanjani akiwa na umri wa miaka 13 tu baada ya kufanya vyema katika Bundesliga ya Vijana chini ya miaka 17 akiwa na Dortmund.

Moukoko aliishia kufunga mara 141 katika michezo 88 pekee kwa timu za Dortmund ya Chini ya miaka 17 na 19 na tayari ameifungia timu ya wakubwa mabao 12 kwenye Bundesliga.



Eduard Camavinga

Fowadi huyo tayari ameshaanza kupata uhakika wa nafasi ya kucheza katika kikosi cha Dortmund na hivi karibuni haitakuwa ajabu kuskia jina lake katika timu ya taifa ya Ujerumani.

**8. Florian Wirtz (Bayer Leverkusen)**

Ikiwa mara kwa mara unafuatilia au unaingia kwenye anga za michezo za qBundesliga basi Florian Wirtz haitakuwa jina geni kwenye rada yako.

Kiungo huyo mkabaji mwenye umri wa miaka 20 ni miongoni mwa tumaini kubwa la soka la Ujerumani baada ya kucheza mechi yake ya kwanza ya ushindani akiwa na Bayer Leverkusen akiwa na umri wa miaka 17.

Kiungo huyu ana Ustadi wa kuchelewa kuingia kwenye boksi na mpiga chenga aliyebobea, Wirtz alirejea kutokana na jeraha baya la goti alilopata katika msimu wa 2021/22 na uhamisho wa pesa nyingi unaweza kuwa kwenye ajenda yake siku zijazo.

**7. Eduardo Camavinga (Real Madrid)**

Ilikuwa Ni ndoto kwa wengi kuchezea Real Madrid na Ufaransa ukiwa na umri wa miaka 20 lakini huo ndio ukweli wa Eduardo Camavinga.



Jamal Musiala

Kiungo huyo huenda anastahili dakika zaidi ya anazopata sasa hivi ,hata hivyo, ni mbadala wa muda mrefu wa Luka Modric, Toni Kroos na Casemiro ambaye tayari ameachwa kwenye safu ya kiungo ya Real, kwa hivyo hana budi kutumia muda wake vizuri.

Camavinga ni mshiriki mkubwa katikati ya uwanja na ana uwezo wa kiufundi wa kutoka nje ya maeneo magumu. Ni supastaa wa siku zijazo ambaye tayari ameshinda Ligi ya Mabingwa, La Liga, UEFA Super Cup na Kombe la Uhispania.

**6. Jamal Musiala (Bayern Munich)**

Jamal Musiala tayari amecheza mechi 90 za Bundesliga akiwa na Bayern Munich na ana umri wa miaka 20 pekee. Pia amefunga mara 23 katika michezo hiyo pia. Inafaa pia kuzingatia kwamba tayari ameshinda Bundesliga na Kombe la Ujerumani mara tatu na pia kuwa na medali za washindi wa Ligi ya Mabingwa na UEFA Super Cup.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, ambaye aliichezea

>>>Inaendelea Uk. 21

# Wanasoka nyota wadogo watakaobadili historia

>>>Inatoka Uk. 20




Uingereza katika ngazi ya vijana lakini akachagua kuitema Three Lions, pia ameichezea nchi yake mechi 23.

Musiala anaweza kufanya kazi kwa upana lakini ni mchezaji bora namba 10. Ana uwezo wa kupata nafasi kati ya uwanja na anaweza kutengeneza na kufunga mabao.

**5. Joško Gvardiol (Man City)**

Joško Gvardiol anatazamiwa kuonyesha ubora wake katika ligi ya tatu akiwa na umri mdogo wa miaka 21 baada ya kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 77 kwenda Manchester City kutoka RB Leipzig katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi.

Uhamisho huo ulimfanya Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia kuwa beki wa pili ghali zaidi duniani na ada kubwa inakuja na matarajio makubwa lakini Gvardiol ana kipawa cha kukidhi matarajio hayo.

Anamfaa Pep Guardiola kwa aina yake ya kustarehe kwenye mpira, uwepo humfanya mpinzani wake kuogopa kuwania mipira ya juu, wakati uwezo wa kucheza katika beki wa kushoto pamoja na nafasi yake ya asili katikati ni ziada ya ubora wake.

**4. Gavi (Barcelona)**

Tunakaribia kuingia kwenye tatu bora na Gavi wa Barcelona kwa bahati mbaya anakosa tu lakini utakapoona wachezaji wetu watatu bora zaidi utaelewa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uhispania, ambaye ameichezea nchi yake mechi 21, tayari ameshaichezea Barcelona zaidi ya mechi 70.

Gavi ana sifa za nguli wa Barcelona Xavi na Andres Iniesta na sasa anaimulika Nou Camp.

Mara nyingi yeye hucheza kama kiungo wa kati na hucheza vyema katika kazi yake ya ulinzi huku pia akiwa mtu sahihi na mwenye maamuzi anapokuwa kwenye mpira.

**3. Bukayo Saka (Arsenal)**

Inaweza kuwa mbaya kwa Bukayo Saka kuwa wa tatu kwenye orodha hii lakini ndivyo ubora unavoamua.

Winga huyo wa Arsenal amekuwa na mvuto tangu alipoingia uwanjani na pia aliwasha moto kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar, na kudhihirisha kuwa anaweza kufanya hivyo kwenye hatua kubwa zaidi.

Mchezaji huyo mnyenyekevu mwenye umri wa miaka 21 kutoka Ealing amecheza zaidi ya mechi 100 akiwa na Arsenal na tayari anajulikana sana. Hebu fikiria kama ataiongoza The Gunners kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu siku zijazo itakuwaje?

**2. Pedri (Barcelona)**

Katika nafasi ya pili ni Pedri wa Barcelona, ambaye kwa sasa amekuwa na kiwango bora sana. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uhispania, kama Gavi, amefananishwa na Xavi na Iniesta.

Pedri ni mseto wa vinara wa Barcelona na anaweza kucheza katikati ya uwanja, kama nambari 10 au hata sita au nane ikiwa inahitajika.

Barcelona wanacheza vizuri zaidi mchezo wao unapopitia kwa Pedri na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 tayari ameshanyakua tuzo za kifahari ikiwa ni pamoja na Mchezaji Chipukizi wa Mashindano ya UEFA mnamo 2020, 2021( Golden Boy )na kuteuliwa katika Timu Bora ya La Liga ya Msimu kwa 2021–22.

**1. Jude Bellingham (Real Madrid)**

Nani mwingine isipokuwa supastaa anayefuata wa England, Jude Bellingham? Kiungo huyo wa kati alikua mchezaji mwenye umri mdogo zaidi katika kikosi cha kwanza cha Birmingham City akiwa na miaka 16 na siku 38 na alicheza mechi 41 za Ubingwa katika klabu yake ya utotoni kabla ya kuhamia Borussia Dortmund.


Bellingham, 20, aling'ara katika Bundesliga kabla ya uhamisho wa kwenda Real Madrid na sasa anatawala La Liga, Ligi ya Mabingwa na kwenye hatua ya kimataifa ya Uingereza.

Aliifungia England kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar na kiungo huyo shupavu na mwenye nguvu, ambaye pia ana ustadi wa kushind. Anaonekana kuwa mtu mashuhuru ajae katika soka la dunia na tunatumai tutamwona akitawala katika Ligi Kuu siku zijazo.

Japo kuna Ushindani kati ya Kylian Mbappe na Erling Haaland na umezungumziwa kama vita kubwa ijayo ya ukuu uwanjani, lakini wachezaji kwenye orodha hapo juu ni kundi litakalofuata la vita ya soka ambao wana umri wa chini ya miaka 21 au chini ya hapo. Na pia wanatizamiwa kufanya makubwa zaidi katika soka siku zijazo.



Josko Gvardiol



Bukayo Saka

# DDC Mlimani Park na somo kwa Vijana utunzi nyimbo za mapenzi

Na Ibrahim Mkamba

KATI ya bendi zote za Tanzania za muziki wa dansi zilizotoa nyimbo zenye ujumbe tofauti wa mapenzi uliowasilishwa kwa lugha adilifu, nimeichagua bendi ya Mlimani Park (wapogoro waliita Milimani Park), wana Sikinde Ngoma ya Ukae, Ngoma Kubwa, Nginde.

Katika tungo zao nyingi za mapenzi, nimechagua sita za ujumbe tofauti ambao ni

1. Kuachana kwa wema kwa kuelezana sababu.
2. Mwanaume kushukuru unapokubaliwa na kushauri muishi vipi mkiwa pamoja na mwanamke aliyekukubali .
3. Kuomba radhi baada ya kupotoka na kuomba nafasi nyingine.
4. Kubembeleza penzi.
5. Kueleza msimamo wako kumhusu umpendae
6. Kumsifu kwa haki umpendae

Hebu tuanze kuzitama tungo hizo.

**1. Kuachana kwa wema na kuelezana sababu za kuachana.**

Wimbo: Penzi la Mwisho

Mtunzi: Joseph Mulenga 1980.

Ujumbe: "Oh dear. Limekuwa ni jambo lisilotegemewa na wengi hasa kwa wanaotufahamu na wetu wazazi pia. Lakini kwangu limekuwa si jambo la ugeni,wala kushangaza, wala kushituka. Ni mimi ambaye nimeishi nawe siku nyingi. Wengineo ni vigumu kufahamu yetu tofauti. Penzi ni kusikilizana si kama hili la sisi."

"Visa, vituko na dharau dada na mengi bila idadi nimevumilia. Kama mapenzi yaua kufa sioni muhali. Usiponipenda wewe,wenzio wanitafuta. Leo nimefika kikomo, naufunga mdomo wangu."

Ujumbe huu umeelekezwa kwa mwanamke ambaye hakuupa thamani uhusiano na mwanaume aliyempenda sana yeye. Licha ya maudhi yote, lakini ujumbe huu hauna maneno makali wala ya kukashfu ukiacha matusi ambayo yasingeweza kupenyezwa. Ni ujumbe uliotolewa kwa lugha ya upole ukijali thamani ya mwanamke na utu wake. Tena ameanza kumueleza kwa kumwita 'Dear' (Mpenzi).

Pia kuna funzo kwamba hata ndani ya mahusiano kuwe na vita vikali namna gani, si vizuri sana vita hivyo kujulikana nje. Hebu soma maneno haya:- "Limekuwa ni jambo lisilotegemewa na wengi. Hasa kwa wanaotufahamu na wetu wazazi pia....ni mimi ambaye nimeishi nawe siku nyingi. Wengineo ni vigumu kufahamu yetu tofauti....." Hapa inaonesha walio nje, wakiwemo wazazi wao, walikuwa wanaona uhusiano huo kuwa haukuwa na tatizo kumbe waliokuwa ndani yake tu ndiyo walijua hali halisi ilikuwaje.




**2. Kushukuru unapokubaliwa na kushauri muishi vipi na mwenzio mkiwa pamoja.**

Wimbo: Pendo Kileo cha Fikara

Mtunzi: Max Bushoke 1984

Ujumbe:- "Penzi ni taji lake mke na mume na hustawi penye mahaba. Pendo kileo cha fikara wala usione ajabu nikisema uliponikubalia tuwe mke na mume nilitamani dunia isimame hata kwa sekunde moja ili nione nuru ya mapenzi yako na roho yangu iwe radhi kuamuru."

"Penzi letu liwe moja kwenye dhiki na faraja, tukiishi vizuri ni shani kwa wapendanao. Ilobaki tusaidiane, tulindiane heshima, tuipende familia ndiyo kustawi kwa pendo."

Ujumbe huu unaeleza umuhimu wa kumshukuru mwanamke anayekubali kujenga nawe mwanaume uhusiano wa kudumu. Shukrani hiyo inaonesha ukubwa wa thamani uliyompa, ukubwa wa thamani ya ombi lako kwake na uzito wa thamani ya kukubali kwake. Siyo akikubali ndiyo basi unajiona wewe mshindi na humtolei kauli yoyote ya kumshukuru. Hapana.

Pia imeelezwa kupitia utunzi huo, haja ya kueleza mapema unataka kujenga mahusiano ya kudumu ya namna gani. Mtunzi ameeleza utaratibu wa kusaidiana, kulindiana heshima na kuipenda familia kati kati ya dhiki na faraja huku penzi likibaki kuwa moja.

**3. Kuomba radhi baada ya kupotoka na kuomba nafasi nyingine.**

Wimbo: Christina Bundala

Mtunzi: Max Bushoke 1984 mwishoni na kusikika zaidi kuanzia 1985 mwanzoni.

Ujumbe: "Ama kweli penzi jamani halikadiriki hata ulipime kwa mzani gani. Nililichezea kamari penzi lake Christina na kujisahau kwamba lingenikaa na kudumu maishani mwangu. Walinirubuni kwa maneno nikamuacha Christina na kujisahau kama angenikaa na kudumu maishani mwangu."

"Niliichezea kamari roho yangu na kuuza utu wangu kwa wasiothamini penzi wala kujua maana ya kupenda. Kwa kweli mpenzi Christina leo naomba unisamehe, nishike uniongoze kwenye penzi letu la haki. Nilihadaika na mambo ya dunia. Nilihadaika na anasa za dunia. Binadamu hujifunza kutokana na makosa."

Ujumbe hapa unaenda sanjari na ule uliowahi kutolewa na wana Saboso, Western Jazz mwaka 1973 wa kuchezea mapenzi ya mtu aliyekuweka juu kimapenzi. Ukikosea, utampoteza na kupata mateso makubwa utakapomhitaji. Wimbo wa Saboso uliitwa Imekuwa Sadaka.

Mtunzi Bushoke anaasa watu kuepuka maneno ya kuwarubuni na matendo mengine ya kuwapotezea wapenzi wa kweli.

Halafu mwenzio akikukosea kama Sikinde walivyomkosea Christina Bundala au Msondo walivyomkosea Mwandani, ni vizuri kutomkomoa kwa kumuumiza akikuomba nafasi nyingine. Muokoe kwa kumsamehe hata kwa masharti ya kutekelezeka. Utajisikiaje ukisikia kafa kwa ajili yako? Utajisikiaje nawe yakikukuta kwa mpenzi wako mwingine na akakataa kukusamehe?

**4. Kubembeleza penzi.**

Wimbo: Kiu ya Jibu

Mtunzi: Max Bushoke 1986

Ujumbe: "Sisemi kwa kuficha, nasema hadharani kinachonifanya nikonde ni kilio cha rohoni na kiu ya kusubiri jibu lako.Kiu ya jibu, kiu ya jibu, kiu ya jibu jamani ndiyo inisumbuayo."

"Tafadhali nijibu jibu ambalo litanirudishia furaha ili roho yangu iweze tulia iwe kama usiku wa mwezi mpevu unaofarijiwa na nyota.Natafuta furaha duniani nimechoka kulala macho kwa kuota ndoto za Alinacha"

"Nilipatapo jibu nasema sitakusumbua. Kumbuka hakuna binadamu duniani asiyejua kutafadhalisha au kutafadhalishwa."

"Tafadhali nijibu nielewe kwa sababu jibu ndilo litanihakikishia, umeipokea samahani yangu ewe Dua."

"Naomba uwe umeridhika kuliachia penzi letu lichanue kama uaridi ili mahaba yatujae rohoni tuwe kama vipepeo, wanaobembelezana."

Hapa kuna ujumbe mzito wa kuomba uhusiano wa kimapenzi uliotengenezwa na maneno adilifu na yenye mvuto mkubwa. Ni sanaa ya hali ya juu mno ya maneno na semi iliyotumika kwenye utunzi huo.

**5. Kueleza msimamo wako kumhusu umpendae**

Wimbo: Conjesta

Mtunzi: Fresh Jumbe/Ally Jamwaka 1987

Ujumbe: "Nimetembea pande nyingi za dunia, Mashariki na Magharibi namtafuta mpenzi mwenye busara ili kujenga mapenzi ya kweli. Na sasa kwako mpenzi nimefikia ukingoni. Sitegemei kupenda mwingine tena zaidi yako we Konjesta."

"Mtoto mwenye imani Konjesta nimeamua kukupenda wewe peke duniani. Niko katika mapenzi mazito sioni mwingine wala sisikii la yeyote yule ila ni wewe. Macho yangu na masikio yangu, mawazo yangu yote ni kwako wewe."

Ujumbe kwa Konjesta unamhakikishia hana mtu anayechangia naye mapenzi. Ni maneno matamu ya kumhakikishia usalama na upekee wake yakitengenezwa kwa umahiri mkubwa wa lugha. Ukimpa mpenzi wako maneno kama hayo, ni wazi atajihisi kama mko naye wawili tu kwenye dunia ya peke yenu.



Max Bushoke (kushoto) na Bennovilla Anthony.

**Nasaha zangu**

Vijana wa sasa mlio wasanii wa nyimbo, hebu fuateni uadilifu wa wataalam hao wa muziki wa dansi. Wametunga nyimbo nyingi nzuri za mapenzi mfano wa hizo sita lakini hakuna ndani yake kuongelewa mambo ya chumbani, kutaja vilivyofichwa ndani ya nguo wala kuongelea migusano na unavyojisikia kwa kuguswa. Wote yule wa penzi la mwisho aliyeitwa Dear, Dua, Conjesta na Naomi wametumika kupitisha ujumbe wa kuvutia wa mapenzi bila kashfa, matusi na udhalilishaji wowote.

Biashara ya muziki sasa ni rahisi mno bila kutumia lugha kali wala za ukakasi. Naomba kuwasilisha, nikiwasihi leo sikilizeni wimbo Naomi wa Nginde, Ngoma Kubwa.



## Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Mtazamo nadhifu wa uso
















Ngozi laini, safi na inayong'aa ni ndoto ambayo sote tumekuwa tukifuatilia tangu tulipobalehe. mabadiliko ya hali ya hewa huleta wasiwasi wa ngozi! Ndiyo, inaweza kuwa vigumu kuonyesha ngozi isiyo na dosari siku nzima kila siku. Kwa kufuata vidokezo rahisi vya urembo kwa uso.

Kunywa maji Ukosefu wa unyevu utaonekana kwenye ngozi yako kwani itaifanya ionekane kavu, yenye kubana na yenye mvuto. Ngozi kavu inakabiliwa zaidi na mikunjo. Kwa kuwa maji hupotea kwa kiasi kikubwa kila siku, unahitaji kuchukua nafasi yake kwa kunywa lita mbili hadi tatu za maji kila siku. Maji huondoa sumu wakati pia hubeba virutubisho kwenye seli. Pia husaidia kupunguza chunusi, alama na hata kuchelewesha mchakato wa kuzeeka.

Osha uso wako mara mbili kwa siku Kuosha uso wako haipaswi kuathiriwa, hata iweje. Inasaidia kuondoa uchafu na uchafu. Na kwa kuosha, tunamaanisha kunyunyiza uso kwa Safi ya Kisafishaji cha Kuzuia Uchafuzi wa Bwawa asubuhi na usiku. Imerutubishwa na kaboni iliyoamilishwa ambayo huondoa athari yoyote ya uharibifu wa uchafuzi wa mazingira. Pia hutibu madoa, chunusi na wepesi kufanya ngozi yako ionekane safi kabisa, isiyo na dosari na yenye kung'aa.

Osha uso na maji baridi. Njia nzuri ya kunyoosha uso wako ni kuosha na maji ya barafu. Hii itarekebisha ngozi yako papo hapo, na kuifanya ionekane safi na yenye afya huku ikiimarisha vinyweleo vyako na kupunguza uwezekano wa kuwa na weusi na chunusi. Inaweza pia kupunguza kasi ya dalili za kuzeeka na kulainisha mikunjo usoni mwako.

Vaa mafuta ya kujikinga na jualJapokuwa kuvaa jua kunaweza kuonekana kama kazi ya ziada isiyoonyesha matokeo ya haraka, kutumia mafuta ya jua leo kutahakikisha kwamba ngozi yako inakushukuru miaka 10 baadaye. Kinga ya jua hulinda ngozi yako dhidi ya miale hatari ya UV na kuzuia makunyanzi, madoa na saratani ya ngozi. Ingawa tunaelewa kuwa vichungi vya jua vinaweza kuwa na grisi, kuna vilivyo na fomula nyepesi ili usijisikie raha.

Tumia kinyago cha uso Usijizuie kuburudishwa kwa barakoa kwa baadhi ya Netflix katika muda wako wa bure. Hata kinyago cha uso cha DIY ni njia rahisi na ya papo hapo ya kupata ngozi yenye afya kama kinyago cha papai kwa ngozi inayong'aa au kinyago cha manjano kwa chunusi.

Pata usingizi wa kutosha Hakuna kulala kwa uzuri sio hadithi. Kulala husawazisha unyevu wa mwili wako na kuweka ngozi yako kuwa na afya. Mwili wako huongeza mtiririko wa damu kwenye ngozi wakati unasinzia, ambayo inamaanisha kuwa unaamka kwa mwanga mzuri. Punguza usingizi na rangi yako inaweza kuonekana isiyo na uhai, yenye majivu, au isiyo na uhai. Ikiwa unataka kulainisha mifuko ya macho yako, makunyanzi na mistari laini, tunapendekeza ufuate kidokezo hiki cha urembo kwa uso na kulala kwa wakati.

Tumia foronya safi. Ikiwa huwezi kukumbuka mara ya mwisho ulipobadilisha kifuniko chako cha mto, basi unapaswa kukibadilisha sasa hivi. Foronya chafu huwa na uchafu mwingi, mafuta na bakteria kutoka kwa nywele, ngozi na shati lako, na zinaweza kusababisha ngozi yako kuzuka. Kwa hivyo, tunapendekeza sana ubadilishe vifuniko vyako vya mito angalau mara moja kwa wiki ili kuona tofauti.

Kujichubua ni lazima. Ikiwa unatafuta vidokezo juu ya jinsi ya kupata uso wazi, jibu sio chochote bali ni exfoliation. inahimiza mzunguko wa damu ambayo inahitajika kwa ngozi ya ngozi na texture laini. Ikiwa hiyo haitoshi, scrub hii haina paraben. Imepakiwa na uji wa shayiri kwa ajili ya kuondoa ngozi nyororo na asali ili kutuliza na kulainisha ngozi.

Finya tu kiasi cha sarafu, usugue usoni mwako kwa upole kisha uifute.Lakini exfoliate mara mbili tu kwa wiki. Kwa kuwa ngozi yako hujisasisha usiku, ni bora kufanywa asubuhi baada ya kuosha uso. Ipendeze ngozi yako kwa masaji nyepesi wakati wa kuchubua kwani kufanya hivyo kutachochea mzunguko wa damu.

Ondoa vipodozi kabla ya kugonga shuka. Jibu la jinsi ya kupata uso safi linatokana na utaratibu wako wa kutunza ngozi wakati wa usiku. Lakini, kabla ya kuamua kulala na vipodozi vyako vyote, hapa ni ukumbusho kwamba inaweza kudhuru ngozi yako Tumia kuondoa vipodozi cha Lakme Absolute Bi-Phased Make-up kwani awamu ya mafuta huondoa haraka hata vipodozi vikali zaidi, wakati awamu ya maji husaidia katika kuburudisha na kulainisha ngozi nyororo na iliyochoka. Kiondoa vipodozi kisichopitisha maji pia kimejaribiwa kwa ngozi na ni salama kabisa kwa watu wenye macho nyeti pia.



Safisha brashi zako za vipodozi mara kwa maraMojawapo ya vidokezo rahisi zaidi vya urembo kwa uso ni kuepuka brashi ambazo hazijaoshwa. Brashi chafu za kujipodoa ni mazalia ya bakteria. Wakati haya yanapogusana na uso wako, husababisha pores kuziba, milipuko na maambukizo mengine kadhaa ya ngozi. Ili kufikia ngozi safi, ni lazima kusafisha brashi yako ya vipodozi kila wakati unapoitumia.

Usitoe chunusi zako. Kutokwa na chunusi kunaweza kushawishi lakini ni uhalifu mkubwa unaofanya. Hualika bakteria kwa uso wako. Je, umewahi kuibua chunusi, na ikarudishwa saa chache baadaye au ukawa na chunusi nyingine karibu nayo? Kweli, yote ni shukrani kwa ujuzi wako wa kutoboa chunusi!

Kwa hivyo, je, fanya ngozi yako na uepuke kugusa chunusi zako Weka mikono yako mbali na uso wako Kugusa uso wako kunaweza kuonekana kama kitendo kisicho na madhara, lakini je, unajua kwamba hii inaweza kuwa mojawapo ya sababu kuu za ngozi yako kuwa wazi? Mikono yetu hukusanya uchafu mwingi siku nzima na tunapogusa uso wetu nayo, tunaishia kuhamisha bakteria kwenye uso wetu. Hivyo, hatua ya kwanza ya kusafisha ngozi ni kuepuka kugusa uso wako mara kadhaa kwa siku.

Fanya mazoezi mara kwa mara. Ingawa wengi wetu tunafanya kazi ili kukaa sawa, pia ni njia ya kupata ngozi inayong'aa! Kufanya mazoezi mara kwa mara huongeza mtiririko wa damu kwa seli za ngozi, na hivyo kupunguza athari mbaya za mkazo wa oksidi. Pia huondoa sumu kutoka kwa mwili, kusafisha ngozi kutoka ndani.

Unaweza kufanya mazoezi nyumbani, kukimbia, kufanya zumba au hata yoga ya nguvu - yote haya hufanya kazi kwa sababu yanafanya mwili wako kusonga, na hilo ndilo lengo. Naam, kwa vidokezo hivi rahisi vya urembo kwa uso nyumbani kama vile kutogusa. uso wako au kuosha vipodozi vyako, sema kwaheri matatizo yako yote ya ngozi kwa muda mfupi.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Novemba 29 - Desemba 05, 2023 |

# Sheria Ngowi ajilipua Jangwani

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNIFU wa kimataifa wa Mitindo wa Tanzania, Sheria Ngowi ambaye amekuwa akifanya kazi na Yanga kwa miaka mitatu sasa amesema hataingia mkataba na klabu nyingine zaidi ya wana Jangwani.

Sheria mbunifu mwenye gharama zaidi Tanzania amesema ameona bora abaki kufanya kazi na Yanga kwa kuwa anachokipata kutoka kwenye klabu hiyo kinamtosha kwenye maisha yake.

Kauli ya Sheria ambaye amewahi kubuni suti za aliyekuwa Rais wa Tanzania, Jakaya Kikwete, ametoa saa chache baada ya Yanga kuzindua jezi mpya za michuano ya Klabu Bingwa Afrika hatua ya Makundi.

"Kwa sasa naona nibaki na Yanga tu, sitafanya kazi ya ubunifu na klabu nyingine yoyote nchini, riziki ninayoipata hapa inanitosha," alisema.

Mbali na kuamua kufanya kazi na Yanga pekee, Sheria amesema ana jezi za miaka mitano ijayo kwa ajili ya timu hiyo ya Wananchi.

# Kumekucha Simba

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Klabu ya Simba, umempa malengo yao Kocha Mkuu mpya wa timu hiyo.

Abdelahak Benchikha aliyetua nchini na wasaidizi wawili, Farid Zemit (Kocha Msaidizi) na Kamal Boudjenane (Kocha wa Viungo) atakuwa nchini kwa misimu miwili.

Jana makocha hao walikutana na Bodi ya Wakurugenzi na baadae Benchi la Ufundi ili kufahamiana.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula alisema wamempa Kocha huyo Uhuru wa kufanya kazi katika kikosi hicho.

"Kocha Farid na Benchikha wamefanya kazi kwa pamoja miaka 30 hivyo jukumu liko kwake kuamua," alisema.

Kwa upande wake Kocha huyo amesema hatangalia jina la mchezaji katika kikosi chake na kutaka ushirikiano kwa ajili ya mafanikio ya Klabu hiyo.

Kocha amesema uwezo ndio utampa mchezaji nafasi sio wapi anatoka.




# Singida FG, Asec Mimosah waunda undugu

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Singida imeamua kutengeneza undugu na klabu ya Asec Mimosah ya Ivory Coast kwa ajili kujifunga mifumo ya ukuzaji vipaji vya wachezaji na uendeshaji wa timu.

Rais wa Singida, Japhet Makau alifanya kikao na Rais wa Asec Mimosas, Ovegnin Francis kwa ajili ya kupata darasa hilo.


Rais Francis, mwenye umri wa miaka 75, amekuwa akiongoza Asec Mimosas kwa zaidi ya miaka 30. Katika kipindi hicho, ameshuhudia wachezaji kadhaa wakubwa wakitayarishwa kwenye Academy ya Asec Mimosas na kwenda kucheza kwa mafanikio makubwa Ulaya.

Miongoni mwa wachezaji hao ni Kolo Toure, Yaya Toure, Didier Zokora, Haruna Dendane, Solomon Kalou, Konate Karim na Diakite Oumar. Hawa ni wachache tu kati ya wachezaji wengi sana waliotokea Asec Mimosas na kucheza kwa mafanikio kote ulimwenguni.

Asec Mimosas ni timu ambayo kila mwaka inauza wachezaji kati ya wanne hadi nane kwa mwaka lakini licha ya kuuza wachezaji wengi, timu hiyo bado inabaki kuwa na nguvu na ina uwezo wa kushindana kimataifa.

Tanzania imefaidika na huduma za ASEC kupitia kwa Ki Aziz, Pacome Zouzou, Kramo, na Yao Yao hata Pascal Wawa alipitia Asec Mimosas.

Rais Makau anafikiria kwenda Abidjan kujifunza zaidi kuhusu Asec Mimosas na jinsi timu hiyo inavyofanya kazi.



# Mtaniona Uwanjani



**Na Mwandishi Wetu**

MLINDA mlango namba moja wa timu ya Yanga, Djigul Diara amesema mashabiki wa klabu hiyo wasiwe na hofu na tatizo lake la bega na watamuona Uwanjani.

Kipa huyo ambaye alianza kukosekana katika kikosi cha Yanga kilichocheza na Coastal Union mjini Tanga na mabingwa hao watetezi kuibuka na ushindi wa mabao mawili, hakuwepo pia kwenye kikosi kilichocheza na CR Belouizdad ya Algeria.

"Nitaonekana Uwanjani, ingawa siwezi kusema lini nimeanza mazoezi na wenzangu kikubwa bega lilihitajika mapumziko kidogo ili kuweza kupona kabisa, si kwamba nilikuwa na tatizo kubwa sana," alisema.

Meneja Habari wa Yanga, Ally Kamwe alisema kuugua kwa mchezaji huyo haikupaswa kuwekwa wazi ili kutowapa nafasi wapinzani.

"Diarra anaendelea vizuri na kama alivyosema ataonekana uwanjani sasa hili nalo ni surprise lakini mashabiki wajue kuwa kipa wao yupo na anaendelea vizuri," alisema.

Yanga watavaana na Mabingwa wa Afrika timu ya Al Ahly ya Misri Jumamosi hii kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

# Mwakinyo afunguliwa, PAF yamng'ang'ania

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHENI ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPRBC), limemfumtia adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja ilichompa bondia Hassan Mwakinyo.

Rais wa Kamisheni hilo, Chaurembo Palasa amesema hatua ya kumfutia kifungo hicho imelenga kusaidia mchezo huo na maisha ya mchezaji huyo kwa kuwa hana shughuli nyingine ya kumuingizia kipato.

Wakati TPRBC ikitangaza kumfungulia Mwakinyo ambaye ilifumngiwa kutokana na kugomea pambano Septemba 29 mwaka huu dhidi ya Julius Indongo wa Namibia, Kampuni ya PAF iliyoandaa pambano hilo bado haijafuta kesi ya madai iliyofungua mahakama kuu.

PAF wanadai fidia kwa hasara ambayo mwanamasumbwi huyo aliwaingiza kutokana na kutotokea Ulingoni huku akiwa ametangaza uamuzi siku mbili kabla ya pambano hilo kupitia mtandao wake wa Instagram.

Mkurugenzi wa PAF, Godson Karigo ameshangazwa pia na hatua ya Kamisheni hiyo kumfunguliwa bondia huyo kabla hajaomba radho hadharani kama makubaliano yalivyokuwa.

Akizungumza hilo Palasa alisema kwanza ilikuwa kumfungulia Mwakinyo linalofuata ni kuomba radhi na ndio maana hata wao hawajamlazimisha Karigo kufuta kesi mahakamani.

